
# Uelekeo

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*


## Yanga kuipasua tena Azam?



**Mwanamke adaiwa kupanga kumuua Rais wa Ukraine**



**Majaji wa UN waamuru Kabuga achiwe**



**Viongozi Afrika Magharibi kuijadili Niger**




| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00024 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Agosti 9 - 15, 2023 |


### KILELE MAONESHO NANENANE:

# Samia aleta kichekokwa wakulima

## ● Apunguza bei ya mbolea ya ruzuku ili kupunguza mzigo

**Lauden Mwambona, Mbeya na Shamila Mkomweke, TURDACo**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameagiza kupunguza Sh. 5,000 kwenye bei ya ruzuku ya mbolea ili kumpunguzia mzigo mkulima.

Hatua hiyo ya Rais Samia, ni pungufu ya bei ambayo Waziri wa Kilimo Hussein Bashe, alitangaza bei ya juu ya mfuko mmoja wa mbolea hiyo kuwa Sh. 85,000.

Mwaka jana, bei ya mfuko mmoja wa mbolea hiyo, iliuzwa kwa Sh. 70,000.

**Inaendelea Uk. 4**



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akikagua moja ya mabanda kwenye kilele cha Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima Nanenane yaliyofanyika kitaifa katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya jana.

Picha: Ikulu.

2 | Habari



**Balozi wa Msumbiji amfagilia Dk. Samia**

3 | Habari



**Mitungi ya gesi 500 yamwagwa jimboni**

5 | Habari



**Polisi wapewa maarifa**

12 | Makala



**Bandari kuchangia nusu ya bajeti serikali**

# Balozi wa Msumbiji amfagilia Dk. Samia

**Na Lauden Mwambona, Mbeya**

BALOZI wa Msumbiji nchini, Ricardo Mtumbuida, ameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendeleza na kuimarisha utaratibu wa Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima Nananane yanayolenga kutoa elimu ya kilimo.

Alitoa pongezi hizo katika Uwanja wa John Mwakangale jijini Mbeya juzi ambako maonesho hayo yanafanyika baada ya kutembelea mabanda mbalimbali yakiwamo ya Halmashauri za Mbozi na Songwe.

Akiwa kwenye Banda la Songwe, aliliambia gazeti la UELEKEO kwamba amejifunza mambo mengi mazuri kwenye maonesho hayo.

Alisema maonesho hayo ni elimu nzuri kwa wakulima, wafugaji na wadau wote wa kilimo jambo ambalo alisema ni la kuipongeza Serikali ya Tanzania chini ya Rais Samia ambayo inaonyesha dhamira ya wazi kuendeleza kilimo nchini.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Solomon Itunda alimshukuru balozi huyo kwa kutembelea banda lake na maonesho hayo kwa jumla.

Akiwa kwenye banda la Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Balozi huyo alijionea vitu mbalimbali vilivyomo ndani ya banda ikiwamo kahawa ya Mbozi na wasindikaji wake.

## Watumishi Ardhi wapewe neno

**Na Mwandishi Wetu, Mbeya**

WATUMISHI wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wametakiwa kufanya kazi kulingana na kasi inayotakiwa na serikali ili kumaliza migogoro ya ardhi inayowakabili wananchi.

Wito huo ulitolewa na Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Shamata Khamis.

Alikuwa akizungumza jana baada ya kutembelea banda la Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwenye Maonesho ya Wakulima na Wafugaji yanayofanyika katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.

Alisema licha ya jitihada kubwa zinazofanywa na watumishi wa wizara hiyo, lakini bado kuna baadhi ya migogoro ya ardhi inayowahangaisha wananchi.

Khamis alisema wizara iendelee kuwaelimisha wananchi hususani wa vijijini ili wafahamu nini mipango na mikakati ya kitaifa ya serikali na utaratibu wa kumiliki ardhi na mwananchi anatakiwa atumie ardhi kwa maendeleo.

"Serikali inafanya kazi kwa niaba ya wananchi na wananchi walio wengi, wanahitaji kuelimishwa ni kwa vipi waitumie raslimali ardhi kwa maendeleo na ili hayo yote yafanyike, lazima kuhakikisha kero zao zinapatiwa ufumbuzi," alisema.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, akizungumza na Makamu wa Rais wa Uganda, Jessica Alupo, kando ya Mkutano wa Pili wa Wakuu wa Serikali wa Nchi 25 za Afrika Wanachama Wazalishaji wa Kahawa unaofanyika Kampala, Uganda. (Picha: Ikulu).

# Tanzania, Marekani zazindua kampeni 'Usingizi wa starehe'

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani, zimezindua kampeni ya ugawaji wa vyandarua vyenye dawa kwenye kaya ikiwa ni jitihada za pamoja katika mapambano dhidi ya malaria nchini Tanzania.

Kupitia kampeni hii inayojitambulisha kwa jina la 'Usingizi wa starehe' itasambaza vyandarua milioni 3.7 vyenye dawa katika kaya za Mkoa wa Kagera na Tabora.

Kupitia ufadhili wa Mfuko wa Rais wa Marekani wa kupambana na Malaria (PMI), Serikali yake inafurahia kufanya kazi kwa ushirikiano mzuri na Tanzania pamoja na wadau mbalimbali katika utekelezaji wa afua mbalimbali za malaria ikiwa na lengo la kuwalinda wananchi wake dhidi ya malaria na hivyo kuchangia katika kupunguza ugonjwa na vifo vitokanavyo na ugonjwa huu.

"Tumekutana, tunasimama kwa pamoja katika dhamira yetu ya kupambana na ugonjwa wa malaria nchini Tanzania. Tunapozindua kampeni ya ugawaji vyandarua vyenye dawa katika kaya za Mikoa ya Kagera na Tabora. Tunatambua ushiriki wa washirika wetu, ikiwa ni pamoja na Serikali ya Marekani, pamoja wadau wengine wa maendeleo, katika juhudi zetu za pamoja za kupambana na malaria," alisema Naibu Waziri wa Afya na kuongeza:

"Kubadilisha vyandarua vilivyochakaa na kuhakikisha upatikanaji wa vyandarua vipya, tunaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa maambukizi ya malaria na kulinda afya za jamii zetu."

Naye Mshauri Mkazi wa Masuala ya Malaria kutoka USAID, Naomi Serbantez, alisema kupitia kampeni hiyo, Marekani inasisitiza dhamira yake ya kuendelea kuisaidia Tanzania katika mapambano dhidi ya malaria na kuboresha afya na ustawi wa watanzania.

"Serikali ya Marekani inafurahi kuungana na wadau wetu wa malaria katika kuzindua kampeni hii ugawaji wa vyandarua vilivyotiwa dawa kwa jamii.

Kwa kuhakikisha kuwa kaya zinapata vyandarua, na vyandarua hivi vinatumiwa kwa usahihi ili kupunguza kwa kiasi kikubwa maambukizi ya malaria na kuwalinda watu walio katika mazingira hatarishi," alisema Serbantez.

# Mitungi ya gesi 500 yamwagwa jimboni



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kaskazini, Exaud Kigahe (kulia), akigawa moja ya mitungi ya gesi kwa mmoja wa wanawake waliohudhuria kongamano la mafunzo ya nishati mbadala ya kupikia kwa wanawake wa jimbo hilo. (Picha: Mpigapicha Wetu)

**Na Doreen Magary**

MBUNGE wa Jimbo la Mufindi Kaskazini ambaye pia ni Naibu Waziri katika Wizara ya Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, amekabidhi mitungi 500 ya gesi kwa wanawake wa jimbo hilo yenye thamani ya Sh. milioni 50.

Fedha za kununua mitungi hiyo ya gesi, zilitolewa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Katika makabidhiano hayo, Naibu Waziri Kigahe, alisema amejipanga vizuri kumuunga mkono Rais Dk. Samia katika kutunza mazingira na kuondokana na uharibifu kwa kuendelea kuwawezesha wananchi na kuwahamasisha kutumia nishati safi kwa wanawake wa jimbo hilo.

Akizungumza jimboni huko wakati wa kongamano la mafunzo ya nishati mbadala ya kupikia (gesi), Kigahe alimshukuru Rais Dk. Samia kwa kutoa fedha za kununua mitungi hiyo kwa ajili ya wananchi na kuahidi kuendelea kumuunga mkono kwa kuhamasisha nafasi hiyo.

"Tunamshukuru sana Rais Dk. Samia, kwa upendo wake huu mkubwa alionao, changamoto iliyopo ni mabadiliko ya tabianchi inayotokana na ukataji kuni, mkaa na maendeleo ya viwanda, hivyo kuwasaidia wananchi kuepukana na nishati haribifu," alisema.

Akifungua kongamano hilo, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendegu, alimpongeza mbunge huyo, kuendelea kutekeleza ajenda ya Rais Dk. Samia ya kutunza mazingira kwa kuhamasisha nishati safi ya gesi na mkaa mbadala, kuachana na matumizi ya kuni.

Alisema athari za mabadiliko ya tabianchi zinatokana na uharibifu wa mazingira ya ukataji kuni za kupikia na kutengeneza mkaa.

# ...4,000 yauzwa bei poa



**Na Mwandishi Wetu, Mbeya**

SERIKALI kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), imeleta mitungi midogo 4,000 ya gesi ya kupikia ili kuuza kwa bei ndogo kwenye Maonesho ya Nanenane jijini Mbeya.

Mitungi hiyo ni ya kampuni za Oryx Gas, Taifa Gas, O-Gas na Lake Gas.

Ofisa Uhusiano wa REA, Joina Msuya, alisema mitungi hiyo ni sehemu ya mitungi mingi ambayo serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imeilipia ili wananchi wanunue kwa bei nafuu kupata nishati mbadala wa kuni na mkaa.

Joina alisema mitungi hiyo ni ya kampuni nne na kwamba itauzwa kwa siku zote za maonesho ya Nanenane.

Mitungi hiyo imewekwa kwenye Banda la Wizara ya Nishati eneo la Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ambapo inauzwa kati ya Sh. 20,000 na Sh. 23,000 kwa mtungi mmoja wenye gesi.

Kwa kawaida, mtungi wa aina hiyo huuzwa kati ya Sh. 44,000 na Sh. 48,000.

# Balozi aihamasisha Zambia kuitumia Bandari D`Salaam



**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI wa Tanzania nchini Zambia, Luteni Jenerali Mathew Mkingule, ametoa wito kwa Jumuiya ya Wafanyabiashara nchini Zambia na nchi za SADC kuendelea kutumia Bandari za Tanzania na hasa Bandari ya Dar es Salaam.

Balozi Mkingule amesema Bandari ya Dar es Salaam ina mchango mkubwa katika sekta ya uchukuzi kwa Tanzania na nchi jirani ikiwemo Zambia.

Alitoa wito huo mwishoni mwa wiki alipotembelea banda la Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), ambayo inashiriki katika Maonyesho ya 95 ya Kilimo na Biashara yanayofanyika Lusaka Nchini Zambia.

TPA inashiriki katika maonyesho hayo kama moja ya Kampeni za Kimasoko na Elimu kwa Umma na wadau zenye lengo la kutangaza huduma za TPA ili kuongeza idadi ya wateja na kiwango cha Shehena katika Bandari za TPA

Luteni Jenerali Mkingule alitembelea Banda la TPA katika maonesho hayo n kuipongeza TPA kwa kudhamini na kushiriki katika maonyesho hayo.

"Wafanyabiashara wa Zambia na nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (SADC), zinapaswa kuendelea kutumia Bandari za Tanzania na hasa Bandari Kuu ya Dar es Salaam ambayo ina mchango mkubwa katika sekta ya uchukuzi na kuna maboresho makubwa sana yamefanyika na yanaendelea kufanyika," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Masoko na Uhusiano wa (TPA), Dk. George Fasha, alisema Zambia ni miongoni mwa nchi ambazo zimekuwa zikipitisha mizigo mingi kwenye Bandari ya Dar es Salaam, lakini pia TPA imefungua ofisi katika nchi hiyo ili kutoa huduma kwa ukaribu kwa wananchi wa Zambia.

"Tumekuja mahsusi kuwaeleza kwamba tuko tayari kuwahudumia na tayari tumeshafungua ofisi hapa nchini kwao na wale wote wenye kutaka maelezo au wenye changamoto basi wafike kwenye ofisi zetu watapatiwa huduma bora kabisa," alisema.

## KILELE MAONESHO NANENANE:

# Samia aleta kicheko kwa wakulima

## ■ Apunguza bei ya mbolea ya ruzuku



**Inatoka Uk. 1**

Akihutubia taifa kwenye kilele cha Sikukuu ya Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima-Nanenane katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya jana, Rais Samia alizitaka Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha, kuangalia namna ya kupunguza gharama za usambazaji wa mbolea hizo hadi kwa mkulima.

Mapema, akizungumza kabla ya Rais Samia, Waziri Bashe alitangaza kuwa mbolea aina ya NPK itauzwa kati ya Sh. 70,000 na 85,000 wakati mbolea inayozalishwa nchini itauzwa kati ya Sh. 68,000 na 75,000.

Alisema mbolea aina ya CAN, itauzwa kati ya Sh. 60,000 na Sh, 65,000 wakati mbolea aina ya SA itauzwa kati ya Sh. 45,000 na 52,000 kwa mfuko mmoja.

Alisema bei hizo zitaanza kutumika Septemba Mosi, mwaka huu.

Kuhusu uuzaji wa mazao ya chakula nje ya nchi, Rais Samia alifafanua kuwa serikali haijapiga marufuku isipokuwa imeweka mfumo mzuri wa kununua mazao hayo kutoka kwa wakulima ambapo sasa wanunuzi kutoka nje hawataruhusiwa kwenda moja kwa moja na malori yao kununua mazao ya wakulima tena kwa fedha za ndani.

Alisema wanunuzi hao wanatakiwa kununua mazao kwa kuzingatia sheria.

"Serikali haijafunga mipaka bali tunataka uwepo wa mfumo mzuri wa pamoja kusimamia uuzaji nje ya nchi utakaomnufaisha mkulima.

Alisema kisheria haikubaliki wageni kununua mazao moja kwa moja kutoka kwa wakulima vijijini, bali lazima wapitie serikalini.

"Kilichokuwepo awali ni kwa mnunuzi kutoka nje kwenda moja kwa moja kwa mkulima shambani na kununua mazao yake tena kwa fedha za kigeni. Tunataka sasa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) w anunue chakula kwa wakulima na wanunuzi wa nje waje kununua kwao," alisema.

Akizungumzia hifadhi ya chakula, Rais Samia alisema anataka hadi ifikapo mwaka 2023, uwezo wa Taifa wa kuhifadhi chakula ufike tani milioni 3 kwa mwaka tofauti na sasa ambapo alisema uwezo wa kuhifadhi chakula ni mdogo.

Alisema serikali imenunua madume 1,160 ya mbegu bora kwa ajili ya nyama na maziwa na pia mkakati uliopo upo pia katika ufugaji wa kuku kwa kuelekeza uzalishaji wa vifaranga ili kuongeza zaidi uzalishaji.

Kuhusu ufugaji, aliwataka wafugaji kuendelea na zoezi la kujisajili pamoja na mifugo yao ili serikali ijue wapo wangapi na mifugo ipo mingapi ili iweze kuwapelekea huduma wanazohitaji.

Kwa upande wa uvuvi, alisema Serikali inatarajia kujenga bandari za uvuvi zenye hadhi ya kimataifa Bagamoyo na Kilwa pamoja na viwanda vya kuchakata samaki.

Aidha alihimiza ufugaji wa viumbe vya majini na mifugo mingine kuwa utanyanyua ajira ya vijana na wanawake nchini.

Mapema, Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, alimpongeza Rais Samia kwa uwekezaji mkubwa anaoufanya katika kilimo cha umwagiliaji, na kilimo kinachofungua fursa kwa vijana kupitia Programu ya mafunzo, mikopo au msaada kwa vijana katika kilimo (BBT).

Aidha, alisema Rais Samia amefanya kazi kubwa ya kuongeza bajeti kwenye utafiti wa kina wa mbegu.

"Bila ya kuwa na utafiti wa kina, huwezi kuwa na uhakika wa uzalishaji mkubwa," alisema.

Alisema kazi hiyo siyo ndogo, inatokana na dhamira kubwa aliyonayo Rais Samia katika kutekeleza Ilani ya CCM hatua ambayo imewafanya Watanzania wengi sasa kupenda kilimo na kukiona kama sehemu ya maisha na furaha yao tofauti na ilivyokuwa awali.

Akizungumzia wafugaji, Chongolo alisema wapo baadhi au kikundi cha watu wenye tabia ya kupeleka mifugo kwenye mashamba ya wakulima na hivyo kusababisha migogoro kati ya pande mbili hizo.

"Wapo baadhi ya wafugaji ambao siyo waaminifu, wameanza kupeleka mifugo kwenye mashamba ya wakulima…na kwa kuwa kila wilaya na mkoa kuna wawakilishi wako, na kama maeneo hayo yatakuwa na viashiria vya migogoro hiyo basi ni dhahiri wawakilishi hao watakuwa hawafanyi kazi zao sawasawa, sasa ni ni vema likatolewa tamko," alisema.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema wananchi wa Mbeya wanamuunga mkono Rais Samia kwa suala la uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema uwekezaji huo utafanikisha kusafirisha bidhaa za wakulima kwenda kuuza nje ya nchi kwa uharaka zaidi.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema kutokana na uamuzi wa Rais Samia kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima, uzalishaji wa mazao ya chakula yaliongezeka kwa tani milioni tatu zaidi.

# Dk. Samia: Kilimo kuendelea kuwa mgongo wa uchumi



**Na Lauden Mwambona, Mbeya**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amesema kilimo kitabaki kuwa uti wa mgongo kwa uchumi wa taifa kama alivyotamka Baba wa Taifa, Hayati Julius Nyerere enzi za uhai wake.

Dk. Samia alitoa kauli hiyo alipohutubia Taifa kwenye kilele cha Maonesho ya Wakulima Nananane uwanja wa John Mwakangale jijini Mbeya jana.

Aidha, alifafanua kuwa Maonesho kama hayo mwakani yatafanyika nmkoani Dodoma.

Vile vile, alisema uwanja wa John Mwakangale, utabomolewa na kujengwa upya kukidhi viwango vya kimataifa.

Kuhusu umuhimu wa kilimo, Rais Dk. Samia alifafanua kuwa serikali yake imeongeza bajeti ya kilimo kutoka karibu Sh. bilioni 250 mwaka 2020/21 hadi zaidi ya Sh. bilioni 970 kwa mwaka 2023/24.

Aidha, aliahidi kuwa serikali yake itaendelea kutoa ruzuku ya mbolea kutokana na kutambua umuhimu wake.

Kadhalika, alisema serikali pia imeanzisha mradi was Building Better Tomorrow(BBT) ili kuimarisha kilimo Biashara nchini na kwamba sasa imeamua kuingia mkataba na JKT ili vijana wazalendo wautekeleza mradi huo.

Katika hatua nyingine, Rais Dk. Samia amemuagiza Waziri wa Kilimo kuanza kufikiria miradi ya umwagiliaji kwa kuchukua maji ya Maziwa Nyasa, Tanganyika na Victoria badala ya kujikita kwenye visima.

Aidha, Rais Dk. Samia alitoa wito kwa wakulima wote nchini kujiwekea akiba ya chakula cha kutosha mwaka mzima kuepuka njaa.

## Polisi wapewa maarifa dhidi ya ukatili kijinsia



**Na Abel Paul, Jeshi la Polisi**

AWAMU ya pili ya wanafunzi wa Jeshi la Polisi wanaochukua kozi ya uofisa wanaendelea kujengewa uwezo na maarifa mapya katika kupambana na ukatili wa kijinsia.

Mafunzo hayo yanaendeshwa kwa pamoja kati ya Kituo cha Utafiti cha Jeshi la Polisi kilichopo Chuo cha Taaluma ya Polisi Dar es Salaam kwa kushirikina na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru (TICD).

Mkuu wa Kitengo cha Utatifi cha Jeshi la Polisi, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Ralph Meela, alisema kazi kubwa ya kituo hicho ni kufanya tafiti na kushirikiana na Taasisi za Elimu ya Juu katika kuwaongezea uwezo maafisa na askari wa Jeshi hilo.

Alisema tayari zaidi ya taasisi 10 zimeshafika chuoni hapo kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa maafisa wanafunzi na wakaguzi wasaidizi wa Polisi huku akimshukuru Mkuu wa Jeshi hilo IGP Camillus Wambura, kwa namna ambavyo amewaunganisha na Taasisi za Elimu ya Juu katika kufanya maboresha ya utendaji kazi unaoendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Kwa upande wake, Mhadhiri Msadizi kutoka Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Elinami Nassari, alibainisha kuwa ni muhimu Jeshi la Polisi kushirikisha jamii na kuzielewa kwa kina jamii ambazo wanakwenda kuzihudumia ambapo aliwaomba maafisa hao wanafunzi kufahamu mila na tamaduni husika ili kutengeneza ushirikishwaji wa jamii kikamilifu na wenye matokeo chanya.

Naye mwanafunzi wa kozi ya uofisa, Rose Mbaga, alisema mafunzo hayo yamewaongezea uwezo na maarifa mapya katika mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Sambamba na hilo, mwanafunzi mwingine Issa Asali, aliwaomba wanafunzi wenzake mara watakapomaliza mafunzo yao na kupangiwa kazi na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, kwenda kutumia njia rafiki walizofundishwa na wahadhiri pamoja na wawezeshaji kutoka taasisi hiyo.

## Wafanyabiashara, maofisa TRA Geita `lugha gongana'

**Na Mwandishi Wetu, Geita**

MAOFISA wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wa Katoro mkoani Geita, wamelalamikiwa kutumia lugha ya Kiingereza kwa wafanyabiashara wanaokwenda kupata huduma katika ofisi hizo, hali inayosababisha kushindwa kuelewana.

Malalamiko ya wafanyabiashara hao yametolewa na wabunge kwenye mkutano wa hadhara katika mji huo mdogo na kudai kuwa wanakutana na changamoto na kupitia wakati mgumu wanapokwenda kufanya malipo ikiwamo kulipia kodi na kukadiriwa kutokana na kutoelewa lugha inayozungumzwa na maofisa wa TRA.

Mbunge wa Jimbo la Geita, Joseph Musukuma, alimlalamikia Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martin Shigella, kwamba hali hiyo inasababisha sintofahamu kwa wafanyabiashara kukadiriwa kodi na ofisi ya TRA Katoro, lakini baadaye wanaibuka maofisa kutoka Geita na kukanusha makadirio ya mwanzo.

"Hapa Katoro tunayo ofisi ndogo ya TRA, maofisa wanakwenda kukadiria kodi wanakubaliana wanaanza kutoa kodi wiki mbili, baadaye wanakuja wengine kutoka Geita wanasema ulikadiriwa kidogo" alisema na kuongeza:

"Mimi napenda kuuliza uhalali au hawa wengine ni maofisa feki ili tuisubiri ile ya Geita, hatuwezi kuwa na wahuni ambao wanafanya kazi halafu baada ya siku mbili, wanakuja wengine wakihoji kitu kile kile."

Naye, Mbunge wa Mbogwe, Nicodemas Maganga, alimuomba Mkuu wa Mkoa huyo, kuangalia suala la wafanyabiashara wadogo wadogo maarufu kama Machinga ambao wapo kwenye soko lisilo na watu, hivyo wapelekwe eneo lenye watu ili wafanye biashara zao vizuri.

Kwa upande wake, Mbunge wa Geita Mjini, Costantine Kanyasu, alisema katika kutekeleza ahadi serikali, inatarajia kujenga shule bora ya Wasichana Geita Mjini, itakayogharimu zaidi ya Sh. bilioni 4.1 kwa ajili kuleta maji na tayari mkandarasi ameanza kazi.

Mbunge wa Bukombe, Dotto Biteko, aliwaomba wakazi Katoro kuacha kusikiliza maneno ya uzushi yanayozungumzwa na wapinzani kwani wanatumia uzushi huo kumuangusha Rais Samia Suluhu Hassan, badala ya kumuunga mkono.

"Nataka niwaambie Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Mama huyu amefanya kazi kubwa sana, hakuna jambo lolote analotaka zaidi ya kuona Tanzania inabadilika. Inawezekana watu hawaelewi kwa sababu ya habari za kusikia. Niwaambie nikiwa shuhuda matendo yake yanamtangaza kuliko anavyosema," alisema Biteko.

Akijibu hoja za Wabunge, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Shigella aliwapongeza wabunge wa mkoa huo kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha maendeleo waliyoyaahidi yanaendelea kufanyika.

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

### Lugha chafu kwa abiria



KUNA baadhi ya makondakta hususan kwenye magari ya abiria yanayofanya safari fupi maarufu kama daladala, wamekuwa na utamaduni wa kutumia lugha za matusi bila kujali mazingira na rika la watu waliopo eneo husika.

Hili si jambo la kiungwana hata kidogo, hasa ukizingatia kuna watoto na watu wa heshima (watu wazima/wenye hadhi tofauti).

Ushauri wangu kwenu ni kuachana na lugha hizo za kifedhuli kwani ni ukiukwaji wa sheria na utamaduni wetu kama Watanzania na kuna adhabu kali kwa wote watakaobainika kufanya hivyo.




MAONI YA MHARIRI

# Dk. Samia ana dhamira ya dhati kuendeleza kilimo

JANA, Rais Samia Suluhu Hassan, aliagiza kupunguza Sh. 5,000 kwenye bei ya ruzuku ya mbolea ili kumpunguzia mzigo mkulima ikiwa ni pungufu ya bei ambayo Waziri wa Kilimo Hussein Bashe alitangaza bei ya juu ya mfuko mmoja wa mbolea hiyo kuwa sh 85,000.

Mwaka jana bei ya mfuko mmoja wa mbolea hiyo ilikuwa ikiuzwa kwa sh 70,000.

Akihutubia taifa kwenye kilele cha Sikukuu ya Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima-Nanenane katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya jana, Rais Samia alisema pamoja na kwamba bei imeongezeka, lakini Wizara ya Kilimo inaweza kuangalia namna ya kupunguza Sh. 5,000 kutoka bei iliyopangwa ya sh 85,000.

Mapema, akizungumza kabla ya Rais Samia, Waziri Bashe alitangaza kuwa mbolea aina ya NPK itauzwa kati ya Sh. 70,000 na 85,000 wakati mbolea inayozalishwa nchini itauzwa kati ya Sh. 68,000 na 75,000.

Alisema mbolea aina ya CAN itauzwa kati ya sh 60,000 na 65,000 wakati mbolea aina ya SA itauzwa kati ya Sh 45,000 na 52000 kwa mfuko mmoja.

Alisema bei hizo zitaanza kutumika Septemba mosi, mwaka huu.

UELEKEO tunachukua nafasi hii, kumpongeza Rais Dk. Samia kwa uamuzi ambao kwa hakika utaleta tija kubwa kwa wakulima.

Kama inavyofahamika kuwa kilimo ni uti wa mgongo kwa uchumi wetu, hivyo ili kuikuza sekta hiyo, hapana budi zichukuliwe hatua za makusudi kama alivyofanya Rais Dk. Samia.

UELEKEO inashauri kuwa, ili hii dhamira njema ya Rais ikamilike, basi wasambazaji wa mbolea kote nchini, watimize wajibu wao kwa kupeleka mapema pembejeo hiyo muhimu kwa wakulima.

Haitapendeza kama wasambazaji watapeleka mbolea kwa wakulima tofauti na wakati inapohitajika, kwani kwa kufanya hivyo ni sawa na kuwahujumu na kulihujumu Taifa lisifikie malengo yake ya kupatikana chakula kwa kila mwananchi.

## Wasiliana nasi


**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000

**Mhariri wa Habari:** +255753333330

**Mhariri Michezo:** +255787559090

**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825

**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam

**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro

**Jengo la:** Aura Mall

**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532

**Email:** uelekeohabari@gmail.com




Na Godfrey Sanga
JICHO LANGU
Sangagodfrey26@gmail.com

# Nanenane nguzo ya uchumi wetu

AGOSTI 8, kila mwaka, Tanzania huadhimisha siku adhimu inayowahusu wakulima, wafugaji na wavuvi.

Ni siku ninayoweza kuiita kwa kifupi kuwa ni sikukuu ya wakulima, wafugaji na wavuvi.

Kilimo kina maana pana inayojumuisha mifumo ya uzalishaji mimea, ufugaji na uvuvi.

Mara nyingi kilimo cha mimea kinaenda sambamba na ufugaji wa wanyama.

Kilimo ni mojawapo ya shughuli za mwanadamu ambayo humsaidia kupata mazao kwa ajili ya chakula na mazao mengine kwa ajili ya biashara ambayo inaweza kumuingizia kipato kwa ajili ya maisha yake, pia kipato hicho husaidia katika kukuza uchumi wa nchi yake ili kujikwamua kiuchumi.

Historia inaeleza kuwa watu walianza kulima takriban miaka 10,000 iliyopita na kabla ya hapo watu waliwinda tu na kukusanya matunda.

Lakini, bado kuna vikundi vidogo na vichache ambavyo vinaendelea na maisha ya kutegemea uwindaji pekee hadi leo, lakini siku hizi zaidi ya asilimia 99 za binadamu hupata chakula kutokana na kilimo.

Inaaminiwa ya kwamba kilimo kilianza katika sehemu tatu za dunia ambako watu walitambua mimea yenye lishe kubwa na kupanda mbegu zake, maeneo haya ambako kilimo kilianza ni China, Amerika ya Kaskazini na Mashariki ya Kati.

Wataalamu hawakubaliani kama kilimo cha Afrika kina asili yake huko Mashariki ya Kati au kama ilianzishwa barani peke yake.

Malengo ya maonesho haya ni kuonesha, kutangaza na kutambulisha kwa mifano mazao mbalimbali yanayozalishwa katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Maonyesho haya kwa mwaka huu yameambatana na kauli mbiu isemayo "Vijana na wanawake ni msingi imara wa mfumo endelevu wa chakula."

Ukitazama kauli mbiu hii utapata picha kutambua kwamba, serikali na Watanzania kwa jumla wana lengo na kusudi kubwa la kufanya kilimo kuwa urithi endelevu kizazi na kizazi kama njia mojawapo inayoweza kuifanya Tanzania kuangaliwa na kuwa tegemezi kwa mambo muhimu hususan chakula kwa mataifa yaliyo mengi, hatimaye uchumi ukaongezeke maradufu zaidi.

> **Ukitazama kauli mbiu hii utapata picha kutambua kwamba, serikali na Watanzania kwa jumla wana lengo na kusudi kubwa la kufanya kilimo kuwa urithi endelevu kizazi na kizazi.**

Jicho langu linaona mengi makubwa kwa miaka michache ijayo katika kukua kiuchumi na kuonekana katika ramani ya dunia kwa kuulisha ulimwengu.

Vijana na wanawake wametajwa kuwa msingi imara katika mfumo endelevu wa chakula. Ukweli ni kwamba hamjachelewa kwani serikali bado ina dhamira ya kufikisha mbali kilimo na watu wake kimaendeleo.

Jicho langu linapongeza, tena linapongeza zaidi jitihada za serikali na taasisi binafsi zinazo unga mkono na kuchangia maendeleo katika sekta ya kilimo kifedha, kielimu na kiuwekezaji na hatimaye kufika hapa tulipofika sasa. Hongera sana.

Ninakukumbusha kijana wa kike na kiume kuwa kilimo ni ajira pekee isiyohitaji mtaji mkubwa wala muda mwingi, tusipoteze muda kuzunguka na vyeti kutafuta ajira na badala yake tujiajiri.

Wewe ofisa ugani uliyeko ofisini, mmeamniwa, nendeni mkatumike kwa vitendo kwakufika mashambani na kutoa elimu kwa wahitaji kwenye kilimo mashambani, jicho langu linaamini Tanzania ya kijani inaundwa nasi sote. Kazi Iendelee.



# Dk. Samia alipia mitungi 4,000 ya gesi Nananane




**Na Lauden Mwambona, Mbeya**

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amesema Rais Samia Suluhu Hassan, amepania kuona Watanzania wanatumia nishati ya kisasa katika kupikia ili kuondokana na karaha ya mkaa na kuni.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wanunuzi wa mitungi ya gesi katika Banda la Wakala wa Nishati Vijijini (REA) lililopo viwanja vya Kimataifa vya Maonesho ya Wakulima Nananane vya John Mwakangale jijini Mbeya juzi.

Alisema Rais Samia ameamua kutoa fedha za kulipia kiasi kwenye mitungi hiyo na hivyo kufanya iuzwe kwa bei ya kati ya Sh. 20,000 na Sh. 23,000 katika viwanja hivyo, badala ya kati ya Sh. 48,000 na Sh. 52,000 kwa bei ya mitaani.

Awali, Ofisa Uhusiano wa REA, Joina Msuya, alisema mitungi 4,000 ya gesi, imetengwa kwa ajili ya kuuzwa Nanenane.

Alisema hata kama itakwisha kabla ya siku Agosti 8, italetwa mitungi mingine.

Mitungi hiyo ni ya kampuni za Oryx, Taifa Gas, O-Gas na Lake Gas.

# Watakiwa kuchangia huduma uzoaji taka

**Na Shamila Mkomweke, TUDARco**

WAKAZI wa Mtaa wa Kidagaa Kata ya Buza, Wilaya ya Temeke jijini Dar es Salaam, wamehimizwa kuchangia huduma ya uzoaji takataka ikiwamo kutoa fedha ili kuepuka magonjwa ya milipuko.

Rai hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa mtaa huo, Shabani Ramadhani, alipozungumza na UELEKEO kwa njia ya simu jana.

Ramadhani alisema mrundikano wa takataka mtaani kwake unatokana na mwitikio mdogo wa wananchi kuchangia malipo ili mkandarasi atimize wajibu wake.

"Zoezi la uzoaji takataka linakuwa gumu hapa mtaani kwangu kutokana na mkandarasi aliyepewa dhamana ya kufanya kazi hiyo, kushindwa kutekeleza kazi yake kwa kushindwa kumlipa kwa sababu wananchi hawashiriki kikamilifu kuchangia huduma hiyo muhimu, hivyo wanatupa takataka hizo kinyemela na kuongeza mrundikano," alisema.

Mwenyekiti Ramadhani alisema uongozi wa mtaa, ulifanikiwa kumtafuta mkandarasi mwingine, lakini changamoto ni fedha za kumlipa.

Aidha, alisema kwa sasa ameandaa mkakati madhubuti kuwabaini wananchi wanaotupa takataka bila kufuata utaratibu ikiwamo na ulipaji wa faini na adhabu kali.

"Nawasisitiza wakazi wangu, tushiriki kikamilifu kuchangia huduma za kijamii kuepusha magonjwa ya mlipuko, tuna mkakati wa kuwadhibiti wale wanaotupa takataka bila utaratibu, watakaobainika watatozwa faini," alisema Mwenyekiti Ramadhani.

Awali, mkazi wa mtaa huo, Chilida Saidi, alisema mtaa wao uko hatarini kupata magonjwa ya mlipuko kutokana na takataka kurundikana bila kuzolewa na kupelekwa mahali sahihi.

> **Zoezi la uzoaji takataka linakuwa gumu hapa mtaani kwangu kutokana na mkandarasi aliyepewa dhamana ya kufanya kazi hiyo, kushindwa kutekeleza kazi yake kwa kushindwa kumlipa kwa sababu wananchi hawashiriki kikamilifu kuchangia huduma hiyo muhimu, hivyo wanatupa takataka hizo kinyemela na kuongeza mrundikano**

# CCM: Wanaolisha mifugo mashambani wadhibitiwe



**Na Mwandishi Wetu, Mbeya**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimewajia juu wafugaji wanaopeleka mifugo kwenye mashamba ya wakulima na kuwataka viongozi wa maeneo husika, wachukue hatua za dhati kukomesha.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, alitoa kauli hiyo alipotoa salamu za Chama mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan, wakasti wa kilele Cha Maonesho ya Wakulima Nanenane yaliyofanyika kitaifa Uwanja wa John Mwakangale jijini Mbeya jana.

Chongolo alisema Watanzania wengi sasa wanapenda kilimo, lakini wafugaji wachache wanapeleka kwa makusudi mifugo kwenye mashamba, jambo ambalo ni hatari kwa usalama.

Aidha, alimpongeza Rais Samia kwa kuthamini kilimo kwa kuongeza bajeti hadi kufikia zaidi ya Sh. bilioni 967 mwaka huu wa fedha.

Pia ameipongeza serikali kwa kuweka mkazo kwenye kilimo cha umwagiliaji na kwamba matunda yameanza kuonekana maeneo mengi.

Naye Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema Wizara yake kwa kushirikiana viongozi wa mikoa, imeanza kuchukua hatua dhidi ya wafugaji wakorofi.

Alitolea mfano akisema wafugaji wa bonde la Kilombero mkoani Morogoro baadhi yao watahamishiwa eneo la Mkata.

Alisema nao Mkoa wa Mbeya umetenga ekari milioni moja ambazo watapewa wenye mifugo watakaotolewa Ihefu.

# Kortini tuhuma kukutwa na kobe wa milioni 116/-



**Na Vivian Victor, TUDARCo**

WATU tisa wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakikabiliwa na tuhuma za kuongoza genge la uhalifu, kuteka wanyama na kumiliki nyara za serikali aina ya kobe 116 wenye thamani ya Sh. 18.9.

Washtakiwa hao walisomewa mashitaka yao na Wakili wa Serikali, Pancransia Protase, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Amir Msumi.

Washtakiwa hao ni Cosmas Ndomba, Josephat Moyo, Deogratius Raphael Lugeng'a, Hamza Juma Abdallah, Kassim Juma Abdallah, Nkanamuli Mhando Mganza, Stephano Elias Chadego, Mwaluko Joshua Mgomole na Olga Kryshtopa.

Wakili Protas alidai katika shitaka la kwanza kati ya Januari na Julai, 2022 walitenda kosa la kuratibu kufanya uhalifu.

Katika shitaka la pili ilidaiwa kuwa washtakiwa walijihusisha shitaka la utekaji nyara wa wanyama pamoja na kununua, kuuza na kusafirisha wanyama aina ya kobe 116.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa shitaka la tatu, washtakiwa wanadaiwa kumiliki nyara za serikali aina ya kobe zenye thamani ya Sh. milioni 18.9 kinyume cha sheria.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa hao walitenda makosa hayo kwa nyakati na mahali tofauti, jijini Dar es Salaam.

Kesi hiyo imepangwa kusikilizwa kesho.

## Mama, mwana kizimbani

**Salimini Mussa na Emeryciana Deus, TUDARCo**

WATU wawili mama na binti yake, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, wakikabiliwa na mashitaka matano ikiwamo matumizi mabaya ya mtandao na kuingilia mfumo wa benki ya CRDB kupitia simu ya mkononi na kufanikisha wizi wa Sh. milioni 13.8.

Washtakiwa hao Riziki Kanena (22) na mama yake mzazi, Laurentina Yustad (43), walisomewa mashitaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Pamela Mazengo.

Ilidaiwa kuwa siku na mahali tofauti jijini Dar es Salaam na Karagwe, mkoani Kagera, washtakiwa waliingilia mfumo wa mtandao wa benki ya CRDB kupitia simu ya mkononi na kufanikisha wizi wa fedha hizo.

Washtakiwa walikana mashitaka hayo na kesi itatajwa kesho kutwa.

## Kizimbani kwa kumsaidia raia wa kigeni kitambulisho

**Salimini Yazidi na Aisha Ramadhani, TUDARCo**

WATU wawili akiwamo raia wa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Fabris Luhamba (32), wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashitaka manne ikiwamo kuishi nchini bila kibali, kutoa maelezo ya uongo kujipatia hati ya kusafiria na kujipatia kitambulisho kwa njia ya uongo.

Mbali na Luhamba, mshtakiwa mwingine ni Hamfrey Mwoyo (37), anakabiliwa na shitaka la kufanikisha kupatikana kitambulisho kwa njia ya uongo na walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Amir Msumi.

Washtakiwa wote walikana mashitaka yao walitakiwa kuwa na wadhamini wawili watakaosaini hati ya dhamana ya Sh. milion moja na kesi hiyo itatajwa tena kesho kutwa.

## Wawili kortini kwa tuhuma kumng'ata mwenzao sikio

**Vivian Victor na Aisha Ramadhani, TUDARCo**

WAHUDUMU wawili, Shamira Issah wa baa na Lucy Salehe wa casino, wamefikishwa Mahakama ya Mwanzo Kariakoo jijini Dar es Salaam, wakikabiliwa na tuhuma za kumpiga na kumng'ata sikio Prisca Mohana.

Washtakiwa hao walisomewa mashitaka yao mbele ya Hakimu Mkazi, Gladness Njau.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa Julai 28, mwaka huu, saa 2:00 usiku, eneo la Clock Tower, Mtaa wa Nkurumah, wilayani Ilala, jijini Dar es Salaam, washtakiwa walimshambulia mlalamikaji kwa kumng'ata sikio na kumsababishia maumivu mwilini.

Hata hivyo, washtakiwa walikana mashitaka hayo na Mahakama iliwapa masharti ya kuwa na wadhamini wawili watakaotia saini hati ya dhamana ya Sh. 300,000.

Hakimu Njau aliahirisha kesi hiyo hadi kesho kutwa, itakapoanza kusikilizwa.

*Leo ndiyo, kesho yetu*

Uelekeo
JARIDA Jumatano Agosti 9 - 15, 2023

# Jungu Kuu







# Maboresho Bandari Dar es Salaam kuchangia nusu ya bajeti ya serikali



UK. 10

## Samia na utekelezaji JNHPP

## Faida za ulaji wa nyanya chungu



UK.

Uchumi

# Samia na utekelezaji JNHPP

- **Aitoa kutoka asilimia 37 hadi 90 ndani ya miaka miwili**
- **Majaribio kufua umeme Februari, uzalishaji kuanza Juni, mwakani**
- **Umeme nchi nzima, utalii kuongezeka, njaa `bye bye'**




**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipoingia madarakani, Machi 19, mwaka 2021, Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) maarufu kama, Bwawa la Nyerere, ulikuwa umefikia asilimia 37. Lakini sasa hivi, mradi huo umefikia asilimia 90, kwa muda wa miaka miwili akiwepo madarakani.

Mradi huo unaotekelezwa kwa gharama ya Sh. trilioni 6.55 ambazo zinagharimiwa na serikali kwa asilimia 100, utakapokamilika, utafuta historia ya tatizo la umeme na kuwapatia Watanzania chakula cha kutosha kwa sababu kutakuwa na mashamba makubwa ya uwekezaji wa uhakika katika kilimo na kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo, yatakayokuwa na miundombinu ya umwagiliaji.

Katika hotuba ya bajeti ya wizara yake Mei mwaka huu, Waziri wa Nishati, January Makamba anasema serikali imeweka azma kusambaza umeme katika vitongoji vyote nchini ndani ya miaka mitano.

Anasema Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ilifanya utambuzi wa wigo wa mradi wa kusambaza umeme katika vitongoji vyote Tanzania Bara na kubaini vitongoji ambavyo bado havijafikiwa na miundombinu ya umeme kuwa ni 36,755 kati ya vitongoji 64,760.

Anasema ili kufikisha miundombinu ya umeme katika vitongoji hivyo, Sh. trilioni 6.7 zinahitajika kwa ajili ya utekelezaji wa azma hiyo.

Akifafanua zaidi kuhusu Bwawa la Nyerere, Waziri Makamba anasema wanatarajia kuanza majaribio ya kuzalisha umeme Februari, mwakani.

Inaendelea Uk.11



# Uchumi



Inatoka Uk.10

Kinachoendelea sasa, Waziri Makamba anasema ni kazi za hapa na pale zinazofanyika kwa kasi kubwa ili kuhakikisha mradi huo unakamilika kabisa ifikapo Juni mwakani.

Anasema kazi ya kufunga mitambo ya kufua umeme inaendelea kwa kasi, huku nyumba inayotumika kusuka mashine, mchakato wake ukiwa umefikia asilimia 70.

Kwa upande wake, Mhandisi Mkazi wa mradi wa JNHPP, Lutenzano Mwandambo, anasema ujazaji wa maji katika bwawa hilo umefikia kina cha mita za ujazo 163. 7 kutoka usawa wa bahari mapema Julai, mwaka huu, kiasi kinachowezesha uzalishaji umeme kuanza.

Kukamilika kwa mradi huo kutawawezesha Watanzania kupata umeme mwingi ambao utasambazwa nchini kote na ziada kuuzwa nje ya nchi ili kulipatia Taifa fedha za kigeni.

Tayari Rais Dk. Samia ameielekeza Wizara ya Uvuvi na Mifugo kuja na mipango mkakati wa ufugaji wa kisasa wa samaki ili kukuza uchumi wa watu wa maeneo haya.

Pia ameielekeza Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, TAMISEMI na mamlaka nyinginezo kupima maeneo hayo kwa kuyaweka kwenye mashamba makubwa kwa ajili ya kufanya mnada wa uwazi kwa wawekezaji wa uhakika katika kilimo, na kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo yatakayokuwa na miundombinu ya umwagiliaji.

Hata hivyo, anatoa angalizo kuwa manufaa ya bwawa hili katika nyanja zote yatawezekana kama tutatunza mazingira katika vyanzo na mabonde ya mito inayoleta maji hapa bwawani.

"Tutunze mazingira maana huu mradi tumeujenga kwa gharama kubwa na kujinyima vitu vingi muhimu, hivyo tuutunze kufa na kupona," anahimiza.

Akiwa mwingi wa shukrani, Rais Dk. Samia, anawashukuru wote walioshiriki kuleta fikra ya mradi huo na katika utekelezaji wake.

Anasema ujenzi wa Bwawa la Nyerere ni kazi kubwa yenye ubora na viwango vinavyotakiwa, safari ya ujenzi ilianza kipindi cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na katika kipindi cha Awamu ya Tano cha Hayati John Pombe Magufuli ujenzi ulianza kutekelezwa, pamoja na mikiki mikiki iliyokuwepo kuhusu suala hili lakini kazi ilianza na kupelekea matunda tunayoyaona hivi leo.

Anasema mradi wa JNHPP utaliletea Taifa umeme wa uhakika kwa ajili ya maendeleo endelevu na kutimiza ndoto iliyokuwepo tangu nchi ilipopata Uhuru.

Anasema mradi huu ni mojawapo ya miradi mikubwa barani Afrika ambao Watanzania wana kila sababu ya kujivunia uwekezaji wake wenye faida nyingi zikiwemo za kuweka akiba kubwa ya maji na kuzalisha umeme hata kama mvua imepungua na kusaidia kudhibiti mafuriko ya mara kwa mara ya Mto Rufiji.

Pia anasema mradi huo utasaidia katika kilimo cha uhakika cha umwagiliaji, utaimarisha na kufungua fursa nyingi za utalii katika eneo la Kusini mwa Tanzania hasa katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na hivyo kutoa ajira za moja kwa moja na nyinginezo.

"Februari, mwakani, tunatarajia kuanza majaribio ya kuzungusha mitambo hiyo," Waziri Makamba anasema alipozungumza na viongozi wa dini waliopata fursa ya kutembelea na kujionea kazi zinazoendelea katika eneo la mradi lilipo Mto Rufiji.

Waziri Makamba anaongeza: "Sasa kazi inaendelea kufanyika usiku na mchana...mradi utakapokamilika utazalisha megawati 2,115 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji."

Anataja faida nyingine za mradi huo kuwa ni pamoja na kuzalisha ajira kwa Watanzania mbalimbali wanaoshiriki katika kuujenga na kutoa huduma mbalimbali kama wauzaji wa vifaa vya ujenzi, mafuta, vyakula na huduma nyingine zinazohitajika kwenye mradi huo.

Tangu kuanza kwa ujenzi wa mradi huo, vigogo mbalimbali kwa nyakati tofauti wamepata fursa ya kuutembelea na kwa Julai, mwaka huu, kundi kubwa la wageni waliopata fursa hiyo ni la viongozi wa dini mbalimbali.

Viongozi hao walielezea kufurahishwa wakisema wanaamini mradi huo ukikamilika na kuanza uzalishaji utakuwa mwarobaini wa kukatika umeme kunakojitokeza mara kwa mara.

Walisema ujenzi wa mradi huo umezingatia na kuheshimu mazingira na kazi kubwa waliyoonayo mbele yao kwa sasa hivi ni kuwahamasisha waamini wao kuhusu utunzaji wa mazingira.



Uchumi

# Maboresho Bandari Dar es Salaam kuchangia nusu ya bajeti ya serikali



**Na Mwandishi Wetu**

MOJA ya matarajio ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ni kuona nusu ya bajeti ya serikali inayopangwa kila mwaka inatolewa na Bandari ya Dar es Salaam.

Kwa maneno yake anasema, "Bandari hii ikifanya vizuri, nusu ya bajeti tunayopanga kila mwaka, itatolewa na Bandari ya Dar es Salaam...nawaomba mjipange vizuri tujenge kwa kasi," alisema Rais Samia alipotembelea bandari hiyo Julai 4, mwaka jana.

Matarajio hayo yanatokana na ukweli kwamba Bandari ya Dar es Salaam, ni lango kuu la biashara na uchumi nchini.

Ingawa zipo bandari nyingine pwani ya Mashariki ya Bahari ya Hindi ndani ya eneo la Tanzania kama vile Mtwara na Tanga; zikiwa pia na Bandari nyingine ndogo zinazotoa huduma katika pwani hiyo kama vile Lindi, Kilwa Masoko, Mafia Kisiwani, Bagamoyo, Pangani na Kwale, bado Bandari ya Dar es Salaam inabaki kuwa lango kuu la biashara na uchumi.

Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) inamiliki bandari zote katika pwani ya Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa pamoja na bandari kavu.

Umaarufu na ukuu wa Bandari ya Dar es Salaam, unatokana na huduma inayotoa siyo tu kwa Tanzania pekee, bali pia kwa nchi jirani zisizo na bahari.

Nchi zisizo na bahari (land locked countries) kwa mfano, Zambia, Burundi, Rwanda, Malawi, Uganda, Zimbabwe, zinahudumiwa na Bandari ya Dar es Salaam.

Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) ina bandari ya Matandi katika Mto Congo, takriban kilomita 150 kutoka Bahari ya Atlantic. Uwezo wa bandari hiyo siyo mkubwa ikilinganishwa na Bandari ya Dar es Salaam ambayo inatajwa kuwa ni ya nne kati ya bandari zote zilizopo pwani ya Bara la Afrika kwenye Bahari za Hindi baada ya Bandari ya Durban, Mombasa na Maputo.

Hivyo, DRC inahudumiwa na Bandari ya Dar es Salaam yenye eneo la

gati 11 zenye kina kirefu hadi mita 14.5 na jumla ya urefu wa mita 2,600.

Tovuti ya bandari hiyo, inaonyesha asilimia 95 ya biashara za kimataifa nchini zinahudumiwa na Bandari hiyo Dar es Salaam. Bandari hiyo inaunganisha Mashariki ya Kati, Mashariki ya Kati, Ulaya na Marekani.

Mwaka 2019/20 makusanyo ya Bandari ya Dar es Salaam, yalikuwa shilingi bilioni 901, mwaka 2020/21 ilikusanya shilingi bilioni 896, na mwaka 2021/22 katika robo ya kwanza ilikusanya Sh. bilioni 980 hadi mwisho wa mwaka.

Umuhimu wa Bandari ya Dar es Salaam unatokana pia na kuongezeka kwa watumiaji wake. Wameongezeka sana kwa sasa.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Mrisho S. Mrisho, ndani ya mwaka mmoja, kwa mfano, wanahudumia magari kati ya 250,000 na kwamba asilimia 60 ya magari hayo, ni ya nchi jirani. Alisema hayo wakati akizungumza na wana habari Mei, mwaka huu.

Hadi hapo mambo yanaonekana kwenda vizuri, ingawa kwenye kila mafanikio changamoto hazikosekani.

Anasema mafanikio ya Bandari ya Dar es Salaam, yanatokana pia na uwepo wa miundombinu ya bandari. Nyenzo zilizopo husaidia uendeshaji wa shughuli za Bandari ya Dar es Salaam.

Kwanza kuna magati ya shehena mchanganyiko (0-5) kwa ajili ya shehena kavu na magari: Gati la makasha (6-7) inayosimamiwa na Bandari ya Dar es Salaam na (8-11) yaliwahi kukodishwa kwa Kampuni ya Kimataifa ya Kuhudumia Makontena (TICTS).

Bandari ina vihenge vya kuhifadhia nafaka vyenye uwezo wa tani 30,000, vituo vya makasha vya nchi kavu vyenye uwezo wa kuhifadhi 24,300 TEUs na CFs yenye uwezo wa kutunza magari 6,000 kwa wakati mmoja.

Pia kuna Single Point Mooring (SPM) yenye uwezo wa kuhudumia meli zinazobeba hadi tani 150,000 za mafuta ghafi na mafuta yaliyosafishwa.

Bomba la Mafuta Kurasini (KOJ) kwa ajili ya bidhaa ambazo zimesafishwa inapokea meli zenye ukubwa wa tani 45,000 (MT) kwa KOJ1 na tani 5,000 kwa KOJ2.

Kwa jumla uwezo halisi wa Bandari ya Dar es Salaam ni kuhudumia zaidi ya tani milioni 18 za shehena kama shehena za kawaida tani milioni 5.2, makasha tani milioni 6.8 na vimiminika tani milioni 6.0.

Kwa upande wa mgawanyiko wa miundombinu ya Bandari, kuna eneo la gati lenye urefu wa mita 2,600 na limegawanywa kwa kuwa na kitengo cha Shehena Mchanganyiko.

Sehemu hii ya bandari ina gati la urefu wa mita 797 lenye mgawanyiko wa magati makuu manne (4), maghala ya kuhifadhia shehena zinazopitia kwenda nchi nyingine yenye ukubwa wa meta za mraba 64,463.5 na hifadhi ya wazi yenye ukubwa wa mita za mraba 201,613.

Kwa miaka kadhaa, sehemu hii iliendeshwa na kampuni binafsi ya huduma za upokeaji na usafirishaji makasha kimataifa Tanzania (TICTS). Kampuni hii ilisimamia shughuli za gati namba 8 – 11. Sehemu hii ina nafasi ya gati ya kutia nanga yenye urefu wa mita 734.

Miundombinu mingine ni vituo viwili vya msaada katika kuhifadhia makasha ambavyo vipo umbali wa kilometa mbili





kutoka bandarini kimoja kipo Kurasini (KICD) na kituo cha Ubungo.

Aidha, Bandari ya Dar es Salaam imetenga gati namba 6-7 yenye urefu wa meta 542 kwa ajili ya kuhudumia makasha.

Bandari ya Dar es Salaam ina miundombinu ya kisasa ya kushughulikia shehena ya nafaka kiautomatiki. Mifumo iliyopo pamoja na vihenge inapokea tani 30,000 za nafaka. Nafaka inaweza kupakuliwa na kujazwa kwenye magunia kwenye eneo la gatini kwa wastani wa zaidi ya tani 2,000 kwa saa 24 au kuhamishwa kwa kutumia malori. Vihenge vipo katika hali inayotakiwa kimataifa ya uhifadhi nafaka.

Kuna maeneo mawili yanayotumika kupakua shehena ya mafuta. Kuna Single Point Mooring (SPM) na Kurasini Oil Jetty (KOJ). Katika eneo la SPM meli ya mafuta hushusha karibu na ufukwe. SPM ina uwezo wa kupokea meli za mafuta zenye uzito hadi tani za metriki 150,000 (MT) na kasi ya kupakua ya kiwango cha mita za ujazo 2,500 kwa saa kwa mafuta ghafi.

SPM imeunganishwa na viwanda vya kusafishia mafuta vya Dar es Salaam na Ndola - Zambia, Eneo jingine ni la Kurasini, KOJ ambalo uhudumia shehena za mafuta yaliyosafishwa ina uwezo wa kusukuma tani 750 kwa saa. Linaweza kushughulikia meli za mafuta hadi zenye tani 45,000 (MT).

Bandari inatoa hifadhi za wazi na zilizofunikwa. Ina vihenge kwa ajili ya nafaka na eneo la kuhifadhia makasha, magari na shehena mchanganyiko.

Bandari ya Dar es Salaam inahudumiwa na boti maalum za kuvutia meli (Tugs), boti za nahodha na boti za ulinzi/doria. Pia kuna miundombinu ya kuelekezea meli bandarini (Navigation Aids). Miundombinu hiyo ni pamoja na maboya, milingoti ya kuongozea meli, alama za ishara na minara ya taa.

Vyombo vikuu vya kuhudumia shehena za kawaida ni winchi kubwa, foko, trekta, matela, grabs, hoppers, Bagging units, malori,mizani, na mikanda ya kuhamishia mizigo.

Bandari ina vifaa vya kuhudumia makasha kama vile winchi kubwa (Ship to shore gantry cranes -SSGs), winchi kubwa za matairi (Rubber tyred gantry cranes RTGs) na winchi kubwa inayotembea katika reli (Rail Mounted Gantry Crane RMG), Gottwalds, malori ya usafirishaji malori yenye foko, matela yanayotumika barabara kuu, matrekta na matela.

## MIRADI MIKUU YA BANDARI.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) inatekeleza miradi mbalimbali kubwa inayotembea katika reli Bandari ya Dar es Salaam kama ilivyoelezwa kwenye utafiti wa mpango mkuu wa Bandari wa Taifa (PMP) uliofanywa na Royal Haskoning, Februari, 2009 na kufanyiwa maboresho mwaka 2020.

Utafiti huo umeweka mkakati wa muda urefu wa Bandari za Tanzania kuwa na uwezo wa kukidhi matarajio ya mahitaji. Miongoni mwa miradi hiyo ni Mradi wa Lango la Bahari la Bandari ya Dar es Salaam (DMGP) ambao utaboresha matumizi na ufanisi kwa kuibadilisha bandari kuwa ya kiwango cha kimataifa yenye ufanisi mkubwa.

Baadhi ya miradi itakayofanya bandari kuwa ya kisasa ni pamoja na kuimarisha na kuongeza kina cha magati ya 1 – 7 na gati la RoRo, uzoaji taka na tope kwenye njia ya kuingilia meli, mzunguko wa kugeuza meli, kuimarisha na kuongeza kina cha magati namba 8 – 11 na kujenga gati jipya la kuhudumia mafuta.

## UBORESHAJI WA UENDESHAJI WA KISASA WA HUDUMA ZA SHEHENA KAVU.

Ndani ya mradi huo TPA itaendesha kisasa shughuli za huduma za shehena kavu kwa kutumia teknolojia ya kisasa yenye ubunifu wa hali ya juu ya usafirishaji.

Ujenzi wa Chelezo.

Hii ni miundombinu kwa ajili ya ukarabati na matengenezo ya vyombo vya kuhudumia meli na hivyo kuongeza ufanisi wa utendaji wa Bandari.

Miradi na maboresho yanayoendelea katika bandari hiyo yanaweza kukidhi shauku ya Serikali kuona nusu ya bajeti inayopangwa kila mwaka itatolewa na Bandari ya Dar es Salaam.

Afya

# Faida za ulaji wa nyanya chungu







Na Godfrey Sanga kwa msaada wa mtandao

LISHE bora ni sehemu muhimu na nyeti katika afya ya binadamu hususani katika kuimarisha mwili na kuulinda dhidi ya magonjwa mbalimbali hasa magonjwa yasiyoambukiza.

Licha ya vyakula vingi kutajwa kuwa na lishe, lakini lishe inayoshauriwa na wataalamu wa afya zaidi ni ulaji wa matunda na mbogamboga kutokana na faida lukuki zinazozopatikana humo.

Leo tunaliangalia tunda linaloitwa nyanya chungu au ngogwe chungu ambalo linatumika zaidi katika mapishi ya aina tofauti.

Tunda hili huitwa (African eggplant), kwa jina la kitaalamu ni Solanum aethiopicum, ni tunda ambalo likipikwa, linaweza kuliwa kama mboga kwenye mlo wa kila siku.

Nyanya chungu vile vile linaweza kuliwa likiwa bichi, likiwa limekaushwa juani au likiwa limeokwa.

Tunda hili pia limekuwa likitajwa na kuhusishwa kwa ukaribu sana na matunda jamii ya bilinganya au Eggplant (aubergine).

Licha ya kuongeza ladha katika chakula, nyanya chungu ina faida nyingi katika kuimarisha mwili wa binadamu kama ifutavyo;

Chanzo kikuu cha vitamin na madini mwilini:

Wataalamu mbalimbali wa lishe kutoka vyanzo tofauti zikiwemo Taasisi za Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), waliwahi kueleza kuwa nyanya chungu au ngogwe, zina umuhimu mkubwa mwilini, hii ni kulingana na uwepo mkubwa wa madini na vitamin kwa wingi.

Waliwahi kusema kuwa vitamini na madini, ni virutubishi vinavyohitajika mwilini kwa ajili ya kuukinga mwili dhidi ya maradhi mengi na kuufanya uwe na afya bora.

Ni ukweli usiopingika kuwa madini na vitamini kwenye nyanya chungu au ngogwe ni muhimu, kwani husaidia kuulinda mwili dhidi ya maradhi.

"Mfano wa madini hayo ni pamoja na madini ya chuma, nyanya chungu au ngogwe ni chanzo kizuri cha madini ya chuma mwilini. aliwahi kunukuliwa.

"Uwepo wa vitamini C kwenye nyanya chungu, husaidia katika ufyonzwaji wa madini ya chuma kwa wingi mwilini na madini ya chuma ni moja ya kirutubishi muhimu katika utengenezaji wa chembe chembe nyekundu za damu na pia madini ya chuma ni muhimu katika kusaidia kusafirishwa kwa hewa ya oksijeni mwilini," alibainisha mtaalamu kutoka TFNC.

Madini ya potashiamu nayo ni muhimu mwilini, kwani husaidia kujenga na kuimarisha misuli ya moyo pamoja na kudhibiti shinikizo la damu na husaidia kuulinda mwili dhidi ya ugonjwa wa kiharusi.

"Madini ya shaba ni muhimu katika uzalishaji wa seli nyekundu za damu ambapo tafiti zinaonesha kuwa madini ya magnesiam ni muhimu katika ukuaji na kuimarisha mifupa dhidi ya dhaifu na iliyovunjika.

"Tafiti zinaonesha kuwa kuna vitamini nyingi kwenye nyanya chungu au gongwe, ikiwa ni pamoja na vitamini A ambayo huyeyuka katika mafuta kwa urahisi na hii vitamin A ni muhimu kwani husaidia kuimarisha mfumo wa kingamwili, kuona vizuri hasa kwenye mwanga hafifu, husaidia kuitengeneza ngozi na kuwa laini na pia husaidia katika ukuaji mzuri wa mwili," aliendelea kueleza.

Wataalamu walisema kuwa vitamin B inayopatikana katika nyanya chungu au ngongwe, ni muhimu katika ufyonzwaji na utumikaji wa mafuta mwilini.

"Kundi la vitamini B, kwa mfano vitamini B1 (thiamine) na vitamini B3 (Niacin au asidi ya Nikotini) na vitamini B6, nayo inapatikana kwenye nyanya chungu au ngogwe.

"Vitamini K ni muhimu katika kusaidia ugandaji wa damu mwilini mfano pindi unapopata katika mwili ambalo litaifanya damu kutoka, basi vitamini K husaidia kuhakikisha haitoki zaidi katika jeraha na hatimaye damu hukata.

"Tafiti zinaonesha kuwa vitamini K ina uwezo mkubwa wa kuzuia ukuaji wa seli za saratani katika mwili wa binadamu na kuimarisha mifupa na pia vitamini K hupunguza magonjwa sugu yasiyo ya kuambukiza kama vile magonjwa ya moyo, baadhi ya saratani na ugonjwa wa kupoteza kumbukumbu "Alzheimer's".

"Tafiti zinaonyesha kuwa na vitamini K za kutosha, huzuia ama kupunguza athari za kupata `stroke', " walinukuliwa baadhi ya wataalamu hao.

Umuhimu wa viondoa sumu vilivyoko kwenye nyanya chungu/ngogwe.

Miongoni mwa faida kubwa ya ngogwe ni ukamilifu wa viondoa sumu yaani `antioxidants' ambavyo hufanya kazi kubwa zaidi katika ulinzi wa mwili dhidi ya magonjwa.

Bado inaelezwa kuwa viondoa sumu vilivyoko katika nyanya chungu au gongwe, ni viini ambavyo vina uwezo wa kuzikinga seli za mwili zisiharibiwe na chembechembe haribifu (free radicals) ambazo husababisha magonjwa ikiwemo saratani.

"Vile vile, kwenye nyanya chungu kuna viini ambavyo huungana na chembechembe hizo haribifu ili kuzidhibiti zisisababishe madhara mwilini.

"Kuna aina mbalimbali za viondoa sumu ambazo kusaidia kuzuia au kupunguza magonjwa sugu yasiyo ya kuambukiza kama vile magonjwa ya moyo na baadhi ya saratani na ugonjwa wa sukari," ilifafanuliwa na wataalamu.

Nyanya chungu au ngogwe zina uwezo wa kudhibiti sukari kwenye damu kwa sababu ya makapimlo au nyuzi nyuzi (fibres) nyingi ambazo husaidia katika umeng'enywaji wa chakula.

"Makapimlo hayo yana umuhimu katika uyeyushwaji wa chakula na kusaidia katika umeng'enywaji na ufyonzwaji wa chakula tumboni, ikiwa ni pamoja na kuzuia mtu kupata choo kigumu (constipation).

"Tafiti zinaonesha kuwa wingi wa makapimlo au nyuzi nyuzi pia husaidia kupunguza kiwango kikubwa cha mafuta ya lehemu (cholesterol) mwilini.

"Tafiti pia zinabainisha kuwa nyanya chungu au ngogwe zina makapimlo kwa wingi hivyo yanaweza kusaidia kupunguza kiwango cha sukari kwenye damu na kuwepo kwa makapimlo kwa wingi na kiwango kidogo cha kalori kwenye nyanya chungu au gongwe, husaidia katika kupunguza uzito.

"Upo utafiti mwingine ambao unaonesha kuwa ulaji wa nyanya chungu mara kwa mara kunaweza kusaidia katika kuulinda mwili na baadhi ya saratani na zingine pia zinaonesha kuwa viini aina ya "solasodine rhamnosyl glycosides, kwenye mimea kama nyanya chungu huweza kusaidia kuulinda mwili dhidi ya baadhi ya saratani," .

Umuhimu wa nyanya chungu katika kufanikisha kazi ya ubongo

Wataalamu wanabainisha kuwa tafiti zinaonesha kuwa kwenye nyanya chungu au ngogwe kuna aina ya kemikali za asili zinazoitwa "phytonutrients", ambazo ni muhimu katika kuboresha afya ya akili.

"Kitendo la kupeleka damu zaidi kwenye ubongo au kuongezeka kwa mzunguko wa damu mwilini, "phytonutrients" husaidia pia kuongeza kumbukumbu kwa kuchochea njia katika "neural pathways" ziweze kukua," ilielezwa na TFNC.

Nyanya chungu hutajwa kuzuia maradhi ya moyo.

Zina kiwango kikubwa cha maji.

Kurekebisha mzungumko wa hedhi kwa wanawake.

Kutibu matatizo ya tumbo la uzazi, kusafisha na kulinda mfuko wa uzazi.

Utalii



# Yajue maisha na maajabu ya nyati

**Kwa msaada wa mtandao**

NYATI au mbogo, ni mnyama wa Afrika. Hana uhusiano wa karibu na nyati maji wa Asia aliye mkubwa zaidi kidogo, lakini asili yake haieleweki. Kutokana na tabia yake isiyotabirika na inayomsababisha kuwa hatari sana kwa binadamu, nyati wa Afrika hafugwi, kinyume cha mwenzake wa Asia.

Nyati ni miongoni mwa wanyama wakubwa. Ana mita 1.7 kwenda juu, urefu wa mita 3.4.

Nyati wa savana ana uzito wa kati ya kilo 500 na 900, ambapo nyati wa kiume kwa kawaida huwa mkubwa kuliko jike, akiwa na uzito mkubwa zaidi. Nyati wa msitu huwa nusu ya kiwango hicho.

Nyati wa savana ni wa rangi nyeusi au kahawia nyeusi na pembe zao zimejikunja katika mpevu, nyati wa msituni nao ni wa rangi ya kahawia nyekundu na pembe zao zimejikunja nyuma na juu.

Ndama wa aina zote mbili wana ngozi nyekundu.

**MAZINGIRA**

Kundi la nyati katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Tanzania.

Nyati wa Afrika ni mmoja wa wanyama maarufu walao nyasi katika Afrika. Wanaishi katika maeneo ya vinamasi, mbuga, na misitu ya milima mikuu ya Afrika.

Nyati hupendelea makazi ya vichaka au matete manene, lakini wanapatikana pia katika mapori ya wazi.

Makundi makubwa ya nyati hupatikana katika maeneo ya miti na mapori. Nyati hawakai katika maeneo yaliyokanyagwa au kupunguzwa kwa muda mrefu.

Nyati huhitaji maji kila siku, kwa hiyo wanategemea vyanzo vya kudumu vya maji.

Kama punda milia, nyati hula manyasi marefu. Nyati hupunguza urefu wa nyasi ili zipendelewe na wanyama wengine walao nyasi.

Wakati wa kula, nyati hutumia ulimi na meno yake mapana kula nyasi haraka kuliko wanyama wengine wa Afrika walao nyasi.

**MAADUI**

Zaidi ya binadamu, nyati huwa na maadui wachache na wana uwezo wa kujikinga na simba na hata kumuua kwa haraka adui yake.

Simba huwaua na kula nyati mara kwa mara, lakini kwa kawaida huchukua simba wengi kumwangusha nyati mzima mmoja.

Mamba wa Nile kwa kawaida hushambulia nyati wazee na ndama tu. Chui na fisi ni tishio tu kwa ndama mchanga, ingawa fisi wameonekana wakiua nyati mzima wakati mara kadhaa.

**TABIA ZA KIJAMII**

Ukubwa wa makundi ya nyati hubadilika sana. Makundi ya kawaida huwa na nyati wa kike wanaohusiana, pamoja na uzao wao, katika ukoo ambao hupangwa kwa hadhi.

Makundi ya kawaida huzungukwa na makundi madogo ya madume ya cheo cha juu, madume ya chini, majike ya cheo cha juu na walio wazee.

Madume vijana hukaa mbali na fahali atawalaye, ambaye hujulikana kutokana na ukubwa wa pembe zake.

**MAFAHALI WANAOJIANDAA KUSHINDANA.**

Mafahali wazima hushiriki katika michezo ya kupigana au vita halisi. Fahali mmoja atakaribia mwenzake, akikoroma, kichwa chake chini, na kusubiri mwenzake kufanya hivyo. Mafahali hao wanapopigana hugeuza pembe zao kushoto na kulia. Ikiwa vita hivyo vina madhumuni ya kucheza, mafahali husuguana uso na miili katika mchezo huu. Vita halisi ni vikali, lakini ni vya nadra na vifupi. Ndama pia wanaweza kushindana, lakini ni nadra kwa nyati wa kike kushindana hivyo.

Wanapokimbizwa na wanyama wa kuwinda, nyati hukaa pamoja kwenye kikundi ili kufanya kuwa ngumu kwa wanyama wa kuwinda kunyang'anya mmoja wao.

Ndama hukusanyika katikati. Nyati atajaribu kumnusuru mwenzake aliyeshikwa. Wito wa ndama hupata uangalifu wa mama na pia kundi lote. Nyati hupigana wakiwa wengi wanapopigana na wanyama wa kuwinda. Wamerekodiwa kuwakimbiza simba juu ya mti na kuwasumbua kwa saa mbili, baada ya simba kuua nyati mwenzao. Inawezekana kwa watoto wa simba kukanyagwa na kuuawa na nyati. Katika tukio lililochukuliwa na picha, ndama alinusurika aliposhambuliwa na simba wachache na mamba baada ya kusaidiwa na kundi.

**UZAZI**

Nyati hujamiiana na kuzaa wakati wa mvua peke yake.

Kilele cha kuzaa huwa mwanzoni wa msimu na kilele cha kujamiiana huwa baadaye.

Fahali atakaa karibu na nyati aliye na joto na pia kuweka mafahali wenzake mbali. Hii ni vigumu kabisa kwani nyati huwavutia madume wengi katika eneo hilo.

Wakati jike yuko tayari kabisa, fahali tu aliye na nguvu kabisa ndiye hubakia kule.

Majike huzaa mara ya kwanza baada ya miaka mitano, baada ya kipindi cha mimba miezi 11.5.

Ndama waliozaliwa hufichwa katika vichaka kwa wiki chache za kwanza wakitunzwa na mama zao kabla ya kujiunga na kundi kuu. Ndama huwa katikati ya kundi kwa ajili ya usalama.[5]

Uhusiano wa mama na ndama hudumu muda mrefu zaidi kuliko wanyama wengi walao majani.

Hata hivyo, wakati ndama mpya anapozaliwa, ule uhusiano unaisha na mama yake huwaweka mbali watoto wengine kwa kutumia pembe.

Nyati wa kiume huacha mama zao wanapokuwa na umri wa miaka miwili na kujiunga na vikundi vya mafahali walio wachanga.

**UHUSIANO NA BINADAMU**

Nyati katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, Tanzania.

Hali ya sasa ya nyati wa Afrika, hutegemea kuwepo wawindaji wa wanyama wa thamani na watalii wawindaji, wakiingilia harakati za kuhifadhi kupitia doria ya urekebishaji wa uharibifu wa mazao kijijini.

**MASHAMBULIZI**

Kama mmoja wa wakubwa watano au kifo cheusi katika Afrika, nyati wa Afrika anajulikana kama mnyama hatari sana, wakiua watu zaidi ya 200 kila mwaka.

Nyati wakati mwingine huripotiwa kuua watu zaidi katika Afrika kuliko mnyama mwingine yeyote, ingawa wakati mwingine hudaiwa kusababishwa na kiboko au mamba.

Nyati huwa na sifa mbaya miongoni mwa wawindaji kama mnyama hatari sana, kwa sababu ya wanyama waliojeruhiwa wakiripotiwa kuvizia na kushambulia wawindaji.

Siasa



# Mapinduzi ya Kijeshi Niger yanaleta sura gani Afrika?

NIGER limekuwa taifa la tano katika ukanda wa Afrika Magharibi kufanya mapinduzi ya kijeshi katika siku za hivi karibuni ikizifuatia nchi za Burkina Faso, Guinea, Mali na Chad. Nchi zote hizo ni makoloni ya zamani ya Ufaransa.

Kutoka mwaka 1990, asilimia 78 ya mapinduzi yote 27 yaliyoshuhudiwa katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara yamefanyika katika nchi ambazo ni makoloni ya zamani ya Ufaransa, hali inayofanya baadhi ya wachambuzi kujiuliza ikiwa Ufaransa – ama urithi wa ukoloni wake – ndiyo wa kulaumiwa kwa kuchochea mapinduzi hayo?

Watekelezaji wa mapinduzi hayo bila shaka wanataka watu waamini kuwa kuna mkono wa Ufaransa. Kanali Abdoulaye Maiga, ambaye alitangazwa kuwa Waziri Mkuu wa mpito wa Mali baada ya jeshi kutwaa madaraka Septemba, 2022 alianza kazi kwa kutoa shutuma kali dhidi ya Ufaransa.

Kanali Maiga aliishutumu Ufaransa kwa kutekeleza, “sera za ukoloni mamboleo, kushusha hadhi (ya nchi za Kiafrika) na visasi,” na kuongeza kuwa nchi hiyo imeusaliti ulimwengu kwa kutokuwa waadilifu na “imeichoma nchi ya Mali kisu mgongoni.”

Kashfa na kejeli dhidi ya Ufaransa pia vimepamba moto katika nchi ya Burkina Faso, ambako Februari, mwaka huu, serikali ya kijeshi ilivunja makubaliano ya muda mrefu ambayo yaliruhusu wanajeshi wa Ufaransa kuendesha operesheni zao nchini humo. Jeshi la Ufaransa lilipewa mwezi mmoja tu kufungasha virago.

Katika nchi ya Niger, ambayo inapakana na Mali na Burkina Faso madai kuwa Rais Mohamed Bazoum, alikuwa ni kibaraka wa Ufaransa yametumika kuhalalisha mapinduzi ya kijeshi dhidi ya utawala wake.

Mikataba mitano ya kijeshi baina ya Niger na Ufaransa tayari imeshavunjwa na kiongozi wa mapinduzi hayo ya juma lililopita, Jenerali Abdourahmane Tchiani. Maandamano ya kuunga mkono mapinduzi hayo yameshuhudia ubalozi wa Ufaransa nchini humo ukishambuliwa na waandamanaji.

Kwa kiasi fulani ushahidi wa kihistoria unaunga mkono baadhi ya madai haya. Utawala wa kikoloni wa Ufaransa ulitengeneza mifumo ya kisiasa ya kuiwezesha kunyakua rasilimali muhimu kutoka kwenye makoloni yake na nchi hiyo imetumia sera kandamizi kuendeleza udhibiti rasilimali hizo.

Hata utawala wa kikoloni wa Uingereza ulitekeleza sera kama hizo. Lakini kinachowatofautisha wakoloni hao wawili, ni namna gani Ufaransa imekita mizizi na kuendelea kuwa na mkono wake barani Afrika, wakosoaji wake wanasema inaingilia moja kwa moja uendeshaji wa siasa na uchumi wa makoloni yake ya zamani hata baada ya uhuru.

Nchi saba kati ya tisa

zilizotawaliwa na Ufaransa katika ukanda wa Afrika Magharibi, bado zinatumia sarafu ya CFA fanc, ambayo mdhamini wake mkuu ni Ufaransa, hii ni sera ya kurithi ya moja kwa moja kiuchumi ya nchi hiyo kwa makoloni yake.

Ufaransa pia iliingia mikataba kadhaa ya kijeshi na makoloni yake ya zamani ambayo ililazimu nchi hiyo kuingilia kati kijeshi na kuwahakikishia usalama wao watawala wa nchi hizo pale walipotaka kung'olewa mamlakani na raia wasiounga mkono tawala hizo.

Kwa kiasi kikubwa, ufadhili na ulinzi wa Ufaransa uliwapa nguvu viongozi mafisadi na madikteta kama Rais wa zamani wa Chad' Idriss Déby na Rais wa zamani wa Burkina, Fasobe Blaise Compaoré, hali ambayo ilifanya mapambano ya kuleta demokrasia katika mataifa hayo kuwa magumu na hatari zaidi.

Ijapokuwa Ufaransa haikuingia mstari wa kati kuwarejesha mamlakani viongozi waliopinduliwa katika siku za hivi karibuni, marais wote waliopinduliwa wamekuwa wakionekana kama wanaunga mkono sera za Ufaransa.

Kibaya zaidi, mahusiano baina ya viongozi wa kisiasa wa Ufaransa na washirika wao barani Afrika umekuwa ukihusisha rushwa na ufisadi na kusababisha kuibuka kwa tabaka la watawala wenye nguvu na utajiri katika nchi ambazo raia wengi wanaishi katika lindi la umasikini.

Mchumi maarufu kutoka Ufaransa, François-Xavier Verschave ndiye mtunzi wa neno Françafrique akielezea mahusiano ya ukoloni mamboleo yaliyojificha katika "siri za kijinai katika ngazi za juu kabisa katika uongozi wa kisiasa na kiuchumi wa Ufaransa. Mahusiano hayo, kwa mujibu wa Verschave, yamesababisha kiwango kikubwa cha fedha "kutwaliwa kifisadi."

Ijapokuwa serikali za Ufaransa za miaka ya karibuni zimekuwa zikijitahidi kujitenga na sera ya Françafrique, kumekuwa na ukumbusho wa mara kwa mara wa uhusiano wa mashaka baina ya Ufaransa, maslahi yake ya kibiashara dhidi maslahi ya bara la Afrika, ikiwemo msururu wa kesi za rushwa na ufisadi.

Hivyo si jambo gumu kuelewa kwanini raia mmoja wa Niger aliiambia BBC kuwa: "Toka utotoni mwangu, nimekuwa nikiipinga Ufaransa… Wamepora utajiri wote wa nchi yetu kama madini ya urani, dhahabu na mafuta."

Kashfa kama hizo zimekuwa zikifichwa nyuma ya pazia wakati viongozi madikteta na washirika wa Ufaransa walipokuwa madarakani, na msaada wa kijeshi wa Ufaransa uliwapa madikteta hao nguvu ya kutuliza mambo.

Katika miaka ya hivi karibuni, uwezo na ushawishi wa Ufaransa pamoja na mataifa mengine ya Magharibi umezorota, hali inayowezesha nchi hizo kushambuliwa na kulaumiwa barani Afrika.

Hali hiyo imedhihirika zaidi pale ambapo viongozi wa kiraia walipong'olewa madarakani na jeshi katika nchi za Burkina Faso na Mali. Kushindwa kwa viongozi hao kuwalinda raia wao dhidi ya tishio la wapiganaji wa kijihadi ikatengeneza taswira kuwa ushirikiano na Ufaransa ni kikwazo na si faida.

Kiwango cha juu juu cha hasira na kukata tamaa cha raia kikawafanya viongozi wa kijeshi kuamini kuwa mapinduzi yatapokelewa kwa shangwe na wananchi.

Hata hivyo, pamoja na makosa yote ambayo Wafaransa wamewatendea makoloni yao barani Afrika kwa miaka yote hiyo, kuzorota kwa amani na demokrasia kunakoendelea kushuhudiwa katika makoloni ya zamani ya Ufaransa haiwezi kulaumiwa Ufaransa pekee kwa kusababisha hali hiyo.

Haikuwa Ufaransa pekee dola yenye nguvu iliyotengeneza na kuwalinda madikteta kuongoza nchi za ughaibuni.

Katika kipindi cha Vita Baridi, Uingereza na Marekani walisaidia kuwaingiza madarakani na kuwalinda madikteta katika nchi kadhaa, kitu cha pekee ambacho walitakiwa kufanya madikteta hao ni kuwa watiifu kwa Marekani na Uingereza. Kuanzia Daniel arap Moi nchini Kenya mpaka Mobutu Sese Seko wa Zaire (sasa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo).

Uhusiano wa karibu baina ya mapinduzi na athari za ukoloni haukonekana katika zama zilizopita. Nchi nne zilizopitia mapinduzi mengi zaidi ya kijeshi barani Afrika toka mwaka 1952 ni Nigeria (8), Ghana (10), Sierra Leone (10) na Sudan (17), zote zilitawaliwa na Uingereza.

Japo msururu wa mapinduzi ya sasa katika makoloni ya zamani ya Ufaransa unaashiria kuwa historia na athari ya sera ya Françafrique inadhihirika, lakini pia mapinduzi hayo yanachochewa na hali isiyomithilika ya kukithiri kwa upotevu wa usalama katika maeneo kadhaa ya Afrika Magharibi na ukanda wa Sahel, ambapo kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa "makundi ya wanamgambo wenye silaha na wenye msimamo mkali," yanafanya wananchi kupoteza imani na serikali za kiraia.

Kila mapinduzi katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita yamechochewa na sababu za kipekee katika mifumo ya kisiasa ya nchi husika. Ni sababu hizo ndizo zilizowagombanisha viongozi wa kiraia na jeshi, na kuwachochea wanajeshi kupoka madaraka pale walipopata upenyo.

Nchini Mali, mazingira yaliyochochea mapinduzi yalianza kujitengeneza baada ya kushamiri kwa wapiganaji wenye msimamo mkali wa kidini baada ya kuanguka kwa serikali ya Libya mwaka 2011, pamoja na madai kuwa rais aliyekuwa madarakani alichakachua uchaguzi na kukua kwa maandamano dhidi ya serikali yaliyoongozwa na vyama vya upinzani katika mji mkuu wa nchi hiyo.

Duru zinaarifu kuwa kilichochochea mapinduzi ya wiki iliyopita nchini Niger ni mipango ya Bazoum kutaka kufumua uongozi wa juu wa jeshi na kumng'oa Jenerali Tchiani kutoka katika wadhifa wake wa mkuu wa majeshi.

Hiyo ni alama tosha kuwa mapinduzi hayo wala hayakuwa na nia ya kuirejeshea Niger mamlaka yake kamili ya kujitawala ama kuwakwamua wananchi kutoka kwenye umasikini bali kulinda maslahi ya maafande wakuu wa jeshi.

Sababu mseto zilizochochea mapinduzi ya miaka ya hivi karibuni pia zinapimika katika kasi ya serikali mpya za kijeshi katika kubadili mahusiano na ushirikiano na dola za kigeni zenye utata.



**"Kwaheri Ufaransa," ndivyo linavyosomeka bango lililokuwa limeshikwa na wafuasi wanaounga mkono mapinduzi.**



**Baadhi ya wale wanaopinga ushiriki wa Ufaransa nchini Niger wameonyesha uungaji mkono wao kwa Urusi badala yake.**

Katika mkutano wa hivi karibuni wa ushirikiano wa Urusi na nchi za Afrika, viongozi wa Burkina Faso na Mali wote walitangaza kumuunga mkono Rais Vladimir Putin na uvamizi wake nchini Ukraine.

Kama ilivyokuwa katika miongo iliyopita, wanufaika wakuu wa mahusiano haya ya kimataifa ni viongozi wakuu wa nchi na si wananchi wa kawaida. Tayari kuna ripoti zinazoonyesha kuwa vikosi vya mamluki vya Wagner vimekuwa vikitekeleza ukatili na mauaji ya mamia ya wananchi nchini Mali kama sehemu ya operesheni yake dhidi ya wanamgambo wa kijihadi.

Hivyo, kupunguza ushawishi wa Ufaransa katika makoloni yake ya zamani hakuwezi kuwa ni mwarobaini wa kuleta utulivu wa kisiasa, na katika miongo kadhaa ijayo tunaweza kushuhudia kizazi kipya cha wanajeshi ambacho kitafanya mapinduzi na kutoa sababu ya kutaka minyororo ya ushawishi wa Urusi katika nchi zao.

***BBC.***

# Kumbukumbu ya shambulio la bomu Ubalozi wa Marekani jijini Dar es Salaam



Pelagia Buberwa

AGOSTI 7, mwaka 1998, wanachama wa kundi la kigaidi la al-Qa'ida (AQ) kwa wakati mmoja, walishambulia kwa mabomu Balozi za Marekani jijini Dar es Salaam, Tanzania na jijini Nairobi nchini Kenya.

Mashambulio hayo mawili, yaliua watu 224 na wengine zaidi ya 4,500 kujeruhiwa pamoja na kusababisha hasara kubwa kwenye majengo ya Balozi hizo na uharibifu wa miundombinu iliyokuwa karibu.

Jijini Dar es Salaam, magaidi walioendesha lori lililobeba vilipukaji, walijaribu kuligonga lango la Ubalozi, wakapiga risasi masijala ya Ubalozi kisha wakalipua vilipukaji.

Mlipuko huo kwa jijini Dar es uliwaua watu 11 na kuwajeruhi 45.

Ni miaka 25 tangu Ubalozi wa Marekani uliposhambuliwa jijini Dar es Salaam.

Lilikuwa shambulio ambalo halikutarajiwa na kwa hakika, lilizua taharuki kubwa kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na kwa Watanzania wote kwa jumla waliozoea amani na utulivu tangu nchi yao ipate Uhuru Desemba 9, mwaka 1961.

Ni shambulio ambalo halitasahaulika kwa Watanzania wengi wa kizazi kile na litaendelea kubaki katika historia ya nchi.

Miongoni mwa Watanzania ambao kumbukumbu ya tukio hilo bado linawasumbua ni Pelagia Buberwa, (pichani), aliyekuwa mmoja wa wafanyakazi wa Ubalozi wa Marekani jijini Dar es Salaam kwa wakati huo.

"Vifo vya wafanyakazi wenzangu, ni jambo ambalo sitasahau kamwe," anasema Pelagia alipozungumza na BBC Swahili.

"Nilikuwa nao asubuhi hiyo; nilizungumza nao, kisha nikatoka kazini na bosi wangu; niliporudi ofisini, walikuwa wameondoka. "Kulikuwa na waathiriwa kadhaa, wengi wao walikuwa wakivuja damu na kulikuwa na hofu kubwa. "Ilinichukua muda mrefu sana nilipokumbuka picha zinanijia mfano dereva wa lori langoni kugongwa na vyuma, nilipofika getini niliona mguu wake upo.

"Kuna mlinzi aliyekuwa akilinda geti, tulipotoka kuelekea kazini na bosi wangu, nilimuaga, lakini tuliporudi baada ya mlipuko huo, nilimkuta amefariki dunia.

"Kulikuwa na mlinzi mwingine ambaye hatimaye alipata ahueni na alikuwa amelala juu ya msichana huyo, akilia bila kujizuia."

Hayo ni baadhi ya maneno ya Pelagia aliyoyasema akikumbuka shambulio hilo lililoacha simulizi kubwa nchini Tanzania.

Katika shambulio la jijini Nairobi siku na muda huo huo, magaidi walilipua lori lililobebeshwa vilipukaji karibu na maegesho ya ubalozi huo na kuwaua watu 213 na awengine 4,500 kujeruhiwa.

Kati ya watu waliouawa, walikuwamo wafanyakazi 44 wa Ubalozi (Wamarekani 12 na raia 32 wa mataifa ya kigeni) — na kuwajeruhi watu wengine 4,500, akiwamo Balozi wa Marekani, Prudence Bushnell.

Wafuatao walishtakiwa na kupatikana na hatia kwenye Mahakama ya Serikali Kuu ya Marekani kuhusiana na mashambulio hayo:

- Mamdouh Mahmud Salim, mwanachama mwanzilishi wa AQ, alikamatwa Septemba, mwaka 1998 nchini Ujerumani na kurejeshwa Marekani. Anatumikia kifungo cha maisha gerezani kwa kuhusiana kwake na mashambulio hayo ya mabomu.
- Oktoba, mwaka 2001, majasusi wa AQ Wadih El-Hage, Khalfan Khamis Mohamed, Mohamed Rashed Daoud Al-Owhali na Mohamed Sadeek Odeh, walipatikana na hatia kwa mashitaka ya kupanga na kutekeleza mashambulio hayo ya mabomu na wakahukumiwa kufungwa maisha gerezani.
- Januari, mwaka 2011, jasusi wa AQ Ahmed Khalfan Ghailani, alipatikana na hatia na akahukumiwa kifungo cha maisha kwa jukumu lake katika mashambulio hayo ya mabomu.
- Septemba, mwaka 2014, Adel Abdel Bari, mshirika wa karibu wa kiongozi wa AQ Ayman al-Zawahiri, alikiri shitaka la kula njama ya kuwaua raia wa Marekani na kupokea kifungo cha miaka 25 gerezani. Aliachiliwa huru kutoka gerezani mwaka 2020.
- . Mei, mwaka 2015, Khaled al-Fawwaz, Naibu wa Kiongozi wa AQ ambaye sasa ni marehemu, Osama bin Laden, alihukumiwa kifungo cha maisha gerezani kwa kuhusiana kwake na mashambulio hayo.


Kenya

Jopo la kusikiliza kesi la Mahakama ya Serikali Kuu, liliwafungulia rasmi mashitaka Abdullah Ahmed Abdullah, Anas al-Libi, Mohammed Atef na Osama bin Ladin kwa majukumu yao katika mashambulio hayo.

Wote wakiwa viongozi muhimu wa zamani wa AQ, sasa ni marehemu.

# Mwanamke adaiwa kupanga kumuua Rais

**KYIV, Ukraine**

IDARA ya Usalama ya Ukraine, imesema mwanamke mmoja amekamatwa kwa madai ya kushirikiana na Urusi na kula njama za kutaka kumuua Rais Volodymyr Zelensky.

Kadhalika, imesema mwanamke huyo kabla, alijaribu kujua ratiba ya Rais Zelensky huko Mykolaiv ambayo ilikumbwa na mafuriko Juni, mwaka huu.

Ukraine mara kwa mara inashutumu wakazi 'wasaliti' wa eneo hilo wanaounga mkono Urusi na kulisaidia jeshi la Moscow kwa kulipa taarifa.

Rais Zelensky alithibitisha kuwa alikuwa amefahamishwa kuhusu kukamatwa kwa mwanamke huyo akisema mkuu wa SBU alikuwa amemjulisha kuhusu vita dhidi ya wasaliti.






## Viongozi A. Magharibi kuijadili Niger

**NIAMEY, Niger**

VIONGOZI wa Afrika Magharibi, wamepanga mkutano utakaofanyika kesho kujadili hatua ya Serikali ya Niger kukataa amri ya kumrejesha madarakani Rais aliyeondolewa kwenye mamlaka na hivyo kuibua matumaini ya kimataifa ya kutafuta suluhu bila ya kutumia nguvu.

Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS), ilikuwa imewaambia viongozi wa mapinduzi ya Julai 26, mwaka huu, kujiuzulu ifikapo Jumapili iliyopita, la sivyo wakabiliwe na uwezekano wa uingiliaji wa kijeshi lakini utawala wa kijeshi, lakini badala yake ulifunga anga ya Niger na kuahidi kuilinda nchi hiyo.

Umoja huo haujajibu moja kwa moja, lakini ulisema Jumatatu utafanya mkutano wa Alhamisi kujadili mkwamo huo uamuzi ambao Umoja wa Ulaya na Marekani zilisema unaruhusu nafasi ya upatanishi.

Akiba ya uranium na mafuta ya Niger na jukumu lake kuu katika vita na wanamgambo wa Kiislamu katika eneo la Sahel vinaipa umuhimu wa kiuchumi na kimkakati kwa Marekani, Ulaya, China na Russia.

## Majaji wa UN waamuru Kabuga achiwe huru

**KIGALI, Rwanda**

MAJAJI wa Umoja wa Mataifa (UN) wameamuru kuwa mshukiwa wa mauaji ya kimbari nchini Rwanda, Félicien Kabuga, aachiwe na kwamba hatua za haraka za kuachiwa huru katika kesi ya uhalifu wa kivita dhidi yake isitishwe kwa muda usiojulikana.

Juni, mwaka huu, Majaji katika mahakama ya uhalifu wa kivita ya UN waliamua kuwa Kabuga hafai kufikishwa mahakamani kutokana na ugonjwa wa akili, lakini walipendekeza taratibu mbadala zifanyike.



Hata hivyo, kwa sasa Majaji wa Rufaa wamekataa pendekezo hili.

Kwa mujibu wa Majaji, Mahakama ya Uhalifu wa kivita ya Umoja wa Mataifa ilifanya 'kosa la sheria' Juni, mwaka huu, kwa kuamua kwamba Kabuga anapaswa kushtakiwa kupitia utaratibu mbadala uliorahisishwa licha ya hali yake ya afya.

Aidha, sasa Mahakama ya Mwanzo imeamrishwa kuhakikisha kabuga anaachiwa.

Mfanyabiashara huyo na mmiliki wa kituo cha redio, kilichotuhumiwa kuhamasisha mauaji ya kimbari, ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 80, ni mmoja wa washukiwa wa mwisho waliosakwa na mahakama hiyo inayochunguza uhalifu uliofanywa wakati wa mauaji ya kimbari ya 1994, nchini Rwanda.

Pia, anatuhumiwa kueneza chuki na mauaji kupitia kituo chake cha redio na kuwahamasisha wauaji waliowaua zaidi ya watu 800,000 katika kipindi cha siku 100.

Alikamatwa mjini Paris, Ufaransa, 2020, baada ya miongo miwili ya kuwa mafichoni, lakini Kabuga alikana mashtaka hayo.

Mahakama imekiri kuwa uamuzi huu wa hivi karibuni, utawakatisha tamaa wahanga na manusura wa mauaji ya kimbari, lakini imebainisha kuwa haki inaweza tu kutendeka kwa heshima kamili kwa haki za watuhumiwa.

BBC.

## Wawili wauawa kwa kupigwa risasi



**CAPE TOWN. Afrika ya Kusini**

WATU wawili wameuawa kwa kupigwa risasi katika siku ya tano ya maandamano ya ghasia katika mji wa Cape Town nchini Afrika Kusini yaliyosababishwa na mzozo wiki iliyopita kati ya madereva wa mabasi madogo na mamlaka.

Polisi wanasema mtu mmoja aliuawa na wengine watatu kujeruhiwa kwa risasi Jumatatu iliyopita karibu na uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Cape Town baada ya waandamanaji kulipiga gari kwa mawe na dereva akajibu kwa kuwafyatulia risasi.

Mtu mmoja alifariki dunia kwa majeraha mengi ya risasi katika shambulizi risasi tofauti.

Ukamataji huo katika kwenye viunga vya mji wa pili kwa ukubwa Afrika Kusini yanafuatia tangazo la Alhamisi iliyopita la mgomo wa wiki moja wa madereva wa mabasi madogo waliokasirishwa na kile wanachokiita mbinu nzito za polisi na mamlaka ya jiji.



# Wema Sepetu aligongea kivazi kwa Ray C

HUU ndio ukweli, kwamba Miss Tanzania 2006 Wema Abraham Sepetu aliazima mavazi ya msanii Rehema Chalamila maarufu kama Ray C wakati wa kampeni za kuwania taji hilo.

Ray C aliyekuwa anatamba wakati na nyimbo Nataka Niwe na Wewe, Uko wapi alililazimika kumuazima Miss Kinondoni huyo na Miss Dar Indian Ocean ili aweze kuimba jukwaani katika shindano la vipaji.

Kwa mujibu wa Ray C, Wema alilazimika kwenda kwake ili kupata nguo kutokana na uamuzi wake wa kutaka kuimba wimbo wa msanii huyo katika shindano la Miss Tanzania Talent.

Kutokana na kuchagua wimbo wa Ray C, aliyekuwa muandaaji wa shindano la Dar Indian Ocean Mange Kimambi alimshauri Wema kuvaa kama msanii huyo na ndipo waliopokwenda kutafuta nguo kwake.

"Wema alifanikiwa kupata viatu na top lakini alishindwa kupata suruali kutokana nay eye kuwa na mapaja makubwa ambazo zangu zisingemtosha… mpaka leo kitop change hakijarudi,"

Msanii huyo ameeleza kuwa yeye na Wema ni marafiki wa muda mrefu. Wema amekuwa ni mpenzi wa muziki kwa muda mrefu na wimbo wa kwanza wa msanii Snura Mushi uitwao Majanga, Wema aliingiza sauti.






# Boyz II Men kupiga shoo Rwanda



**KIGALI, Rwanda**

WAKALI wa muziki wa R&B kundi la Boys II Men la Marekani linatarajiwa kufanya onyesho kubwa la uziki jijini Kigali mwishoni mwa mwezi Oktoba mwaka huu.

Onyesho hilo la wakali wa hao zamani, litafanyika Oktoba 25 katika ukumbi mpya wa burudnai BK Arena.

Kundi hilo lililoanzishwa mwaka 1985, ilikuwa bendi maarufu ya vijana iliyochangia kwa kiasi kikubwa kuanzishwa kwa vikundi vingi vya vijana vya muziki wa R&B katika miaka hiyo.

Boys II Men inaundwa na wanamuziki wanne ambao ni Nathan Morris, Shawn Stalkman na Wanya Morris. Baadhio ya nyimbo maarufu za kundi hilo ni pamoja na "I'll make love to you" na "On Bended Knee".

# Akothee akerwa kuuliza ndoa yake



NYOTA wa muziki wa Kenya, Esther Akoth almaarufu Akothee amekerwa na swali juu ya ndoa yake mpya iliyokuwa ifungwe mwezi uliopita nchini Uswizi.

onekana kukasirika baada ya kuulizwa kuhusu mipango yake ya harusi yake ya pili na mume wake mzungu Denis 'Omosh' Schweizer ambayo ilitakiwa kufanyika nchini Uswizi.

Aprili10 mwaka huu, Akothee alifunga ndoa na kutangaza kuwa watafunga ndoa ya pili nchini Uswizimwezi Julai.

"Madam Boss, hatujasahau harusi yako kubwa, lini?" Shabiki aliuliza.

Msanii huyo mwenye watoto watano alimjibu shabiki huyo kwamba ametengana na mume wake mara baada ya harusi yao ya kwanza iliyofanyika Nairobi Aprili. 10 mwaka huu.

Lakini matarajio ya kufanyika kwa harusi hiyo ya pili ni ya Akothee na mume wake ni makubwa amesema harusi hiyo itahudhuriwa na watoto wake wote isipokuwa watoto wake waliopo shule Ufaransa japo hajasema itafanyika lini.

# Baba Bhoke aoa tena



MWANAMITINDO wa kimataifa wa Tanzania, Frank Mgoyo ama Frank Machozi maarufu pia kama Baba Bhoke amefunga ndoa Jumamosi mjini Dar es Salaam.

Frank aliyekuwa mwanamitindo wa kwanza Mtanzania kutengeneza tangazo nchini Afrika Kusini na baadae kuonekana kwenye wimbo uitwao Machozi wa msanii Judith Wambura.

Frank ambaye alikuwa akifanya kazi na kampuni ya mitindo iitwayo Faces International alipewa jina la Baba Bhoke jina la binti yake wa kwanza aliyezaa na aliyekuwa muandaaji wa shindano la Miss Dar Indian Ocean.

Bhoke amekuwa maarufu zaidi kwenye mitandao ambapo juzi watu walimtumia meseji Mange wakimpa taarifa kuwa mzazi mwenzake anaoa naye akajibu ameagiza Panadol maana kichwa kinamuuma.



# Tottenham yakataa tena Ofa ya Bayern Munich

**LONDON, England**

NDOTO za Bayern Munich bado zipo kwa mshambuliaji Harry Kane kwa ajili ya msimu wa ligi ya Bundesliga licha ya ofa yao ya pili kupigwa chini.

Changamoto kubwa kati ya pande mbili hizo ni juu ya thamani halisi ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 30.

Wababe hao wa Bundesliga wanasema endapo mipango yao itakwama msimu huu kuhusu Kane basi watageukia upande mwingine ili waweze kupata mmaliziaji katika kikosi chao.

Hata hivyo ikiwa zimebaki wiki tatu kabla dirisha la usajili halijafungwa, yapo matumaini huenda suala hilo likamalizika. Kane amefunga mabao 280 katika mechi zote alizoichezea Spurs, ingawa Jumapili hakushiriki kwenye mazoezi.

Kane amebakiza mwaka mmoja katika mkataba huku kukiwahakuna kipengele cha kuongeza mkataba ukimaliza hali ambayo inaifanya klabu hiyo kupoteza uwezekano wa kupata pesa kupitia yeye endapo atamaliza mkataba wake na kuondoka kama mchezaji huru.

***Habari zote zimeandaliwa na Hidaya Machuppa, TUDARCo kwa msaada wa mashirika ya Habari***



# Alvarez akamilisha usaijili leo West Ham

**LONDON, England**

KIUNGO wa Mexico, Edson Alvarez atafanyiwa vipimo kwa ajili ya kukamilisha mipango ya kujiunga na klabu ya West Ham United.

Alvarez amekuwa midomoni mwa mashabiki wa wagonga nyundo hao wa London, mpaka kufikia makubaliano na klabu ya Ajax Amsterdam ya Uholanzi kwa kitita cha paundi milioni 35.

Kiungo huyo alikuwa mmoja wa wachezaji waliokuwa kwenye kikosi cha Mexico kilichoshinda Kombe la la CONCACAF huko Marekani na kwa sasa anaonekana ndio mrithi wa Declan Rice.

Taratibu zingine za uhamisho wa Alvarez zitakamilika leo ingawa kujiunga kwake inaonekana ni ahueni kwa Kocha David Moyes hasa kutokana na pengo la Rice kwenda Arsenal.

# Katie Boutler kukutana na Coco Gauff



Coco Gauff

**LONDON, England**

MCHEZAJI namba moja wa tenisi wa Uingereza, Katie Boulter anatarajiwa kupambana na Coco Gauff katika michuano ya dunia ya mchezo huo itakayofanyika huko Monteal, Canada.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27alifuta ndoto za nyota wa Canada, Rebecca Marino baada ya kumchapa seti mbili kwa bila katika pambano lililochukua saa moja na dakika sita. Katie alishinda kwa 6-3 6-1.

Katie ambaye anashika nafasi ya 72 duaniani anatarajia kushusha bomu nyingine katika pambano hilo baada ya kufanikiwa kuwashinda wapinzani wake wawili katika micghezo ya awali.

Gauff ambaye anashika nafasi ya sita. Kwa upande wake Katie Boulter, hajawji kupoa tangu amkung'ute mchezaji namba 103 duniani, Marino.

Ameshinda mechi kadhaa kwa pointi 3-1 katika mechi kadhaa za muhimu kwake

Katika mechi nyingine Karolina Pliskova atachuana na mchezaji namba moja wa dunia, Iga Swilatek wa Poland . Pliskova raia wa Czech alitumia masaa mawili na dakika 22 kumtandika raia wa China, Zhu Lin 6-3 6-7 (8-10) 6-2.



Katie

# Liverpool nayo yagomewa



**LONDON, England**

OFA ya tatu ya klabu ya Liverpool kwa ajili ya mchezaji wa kiungio, Romeo Lavia (19) imepigwa chini tena na klabu ya Southmpton

Ofa ya mwisho iliyowekwa kwa ajili ya mchezaji huyo inatajwa kiwa paundi milioni 46 huku Southmpton wakitaka mezani millioni 50/

Lavia alikuwa benchi wakatiu Southampton walipoanza kampeni yao ya ligi ya Championship katika mechi yao dhidi ya Sheffield Wednesday ambao walishinda mabao 2-1.

Alijiunga na timu hiyo akitokea Manchester City kwa kitita cha paundi milioni 10.5. na mpaka sasa amecgheza mechi 34 ingawa alisjindwa kuisaidia timu hiyo

# Bondia Grace Mwakamele atwaa Medali



**Na Wemael Mmaraba**

BONDI wa Kimataifa wa Tanzania, Grace Mwakamele ameshika nafasi pili katika mashidano ya Ubingwa wa Afrika yaliyofanyika nchini Cameroon.

Matokeo hayo yamemfanya Grace kuweka rekodi kuwa bondia wa kwanza wa kike wa Tanzania kufika ngazi hiyo.

Grace amepata medali ya fedha huku akivunja rekodi iliyodumu kwa miaka 30 ambapo ndio mara ya mwisho kupata medali ya fedha katika michuano ya Afrika.

Katika michuano hiyo Tanzania ilipata pia medali ya shaba kutoka kwa bondia Shaban Changalawe. Tanzania iliwakilishwa na mabondia watatu katika mashindano hayo.

Baraza la Michezo la Taifa (BMT) limewapongeza mabondia hao kwa kuweza kuipa heshima Tanzania.

# Yanga kuipasua tena Azam?



**Inatoka Uk.24**

Upinzani wa mechi hii unachochewa zaidi na hatua ya Azam kusajili nyota wawili wa Yanga Yanick Bangala Litombo na kiungo Feisal Salum 'Fei Toto'.

Yanga ambayo imefanya mabadiliko kwenye kikosi chake tofauti na kile cha awali kilichocheza na Azam inataka kuendelea kuthibitisha ubora wake si kwa Azam tu bali kwa mashabiki na timu pinzani.

Azam ambayo mwaka huu inaonekana imepania zaidi kufanya vizuri kwa kuanzia na ngao ya Hisani hii inatokana na usajili wake hasa kwa maingizo kutoka Afrika Magharibi. Azam ina nyota kama Gibril Sillah kutoka Gambia, Alasairu Diao na Sheikh Sidibe wa Senegal huku Prince Nkumelelho Dube na James Agaminko wakitaka kudhihirisha ubora wao.

Yanga yenye Skudu Makudubela, Konkon, Pacome Zouzou na wenyeji kama Clement Mzize, Kenneth Musonda watahitaji kuonyesha uwezo wao bila kuwepo kwa Fiston Kalala Mayele.



# Nabi, Kaze 'walifukuzwa kazi' mechi ya Club Africain

**Inatoka Uk.24**

Kauli hiyo imetolewa mshambuliaji wa zamani wa Yanga Fiston Mayele katika Makala maalum ya kuzungumzia safari ya timu hiyo katika mashindano ya CAF.

"Ile mechi ya marudiano dhidi ya Club Africain ilikuwa na presha kubwa! Kwa sababu mchezo wa kwanza tulitoka suluhu Dar, ili tufuzu hatua ya makundi (Kombe la Shirikisho la CAF) tulitakiwa kushinda Tunisia."

"Wakati tunasafiri kwenda Tunisia Kocha Nabi alifunga na alibeba mabegi yake yote. Kocha Kaze alimwambia mkewake afunge mizigo yote na kujiandaa kwa ajili ya kurudi Burundi."

"Wakati huo kulikuwa na tetesi nyingi kuwa Kocha



anafukuzwa na tayari kuna kucha mwingine mpya."

Kauli ya Mayele inaakisi kile ambacho Kocha Nabi aliwahi kuzungumza na gazeti hili na kusema hata ndani ya timu kulikuwa na mgawanyo na hakuna ambaye alitarajia kuwa wangevuka.

Bila kufafanua zaidi Nabi alisema hofu ilikuwa kubwa sana na mpasuko ulikuwa wazi. Yanga ilivuka kwa bao la Aziz Ki ambaye aliingia kutokea benchi.

# Singida Fountain Gate, Ruffo wamgeukia msichana




**Inatoka Uk.24**

Mradi huo una lengo la kushughulikia tofauti za kijinsia na kukuza fursa sawa kwa wanawake na wasichana chini ya miaka 18, wanaojihusisha na soka la Tanzania.

Mkurugnezi wa Singida FG, Rajab Kelvin alisema mradi huo una angalia usalama wa wasichana n vijana katika michezo kutokana na kuwepo wa vipaji vikubwa kwa watu hao.

Timu hiyo imesema kupitia mradi huo idadi ya wasichana watakaojiingiza kwenye michezo itaongezeka zaidi kutokana na kuona thamani na usalama wa mazingira watakayokuwepo.

**Inatoka Uk.20**

| R | M/N | DATE | HOME TEAM | | AWAY TEAM | TIME | VENUE | REGION |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ROUND 28 | 217 | May 17, 2024 | Kitayosce FC | vs | Ihefu FC | 16:00 | Ali Hassan Mwinyi | Tabora |
| | 218 | May 17, 2024 | Kagera Sugar FC | vs | Coastal Union FC | 19:00 | Kaitaba Stadium | Kagera |
| | 219 | May 18, 2024 | Tanzania Prisons FC | vs | Mashujaa FC | 16:00 | Sokoine Stadium | Mbeya |
| | 220 | May 19, 2024 | Mtibwa Sugar FC | vs | Namungo FC | 16:00 | Manungu Stadium | Morogoro |
| | 221 | TBA | Dodoma Jiji FC | vs | Young Africans SC | TBC | Jamhuri Stadium | Dodoma |
| | 222 | TBA | JKT Tanzania FC | vs | Azam FC | TBC | Black Rhino Stadium | Arusha |
| | 223 | TBA | Simba SC | vs | Geita Gold FC | TBC | Benjamin Mkapa | Dar es Salaam |
| | 224 | TBA | KMC FC | vs | Singida BS FC | TBC | Uhuru Stadium | Dar es Salaam |
| CAF CL FINAL (24 - 26 May) 2nd Leg | | | | | | | | |
| ROUND 29 | 225 | TBA | Coastal Union FC | vs | JKT Tanzania FC | TBC | Mkwakwani Stadium | Tanga |
| | 226 | TBA | Simba SC | vs | KMC FC | TBC | Benjamin Mkapa | Dar es Salaam |
| | 227 | TBA | Ihefu FC | vs | Dodoma Jiji FC | TBC | Highland Estates | Mbeya |
| | 228 | TBA | Mashujaa FC | vs | Mtibwa Sugar FC | TBC | Lake Tanganyika | Kigoma |
| | 229 | TBA | Namungo FC | vs | Tanzania Prisons FC | TBC | Majaliwa Stadium | Lindi |
| | 230 | TBA | Young Africans SC | vs | Kitayosce FC | TBC | Benjamin Mkapa | Dar es Salaam |
| | 231 | TBA | Singida BS FC | vs | Geita Gold FC | TBC | Liti Stadium | Singida |
| | 232 | TBA | Azam FC | vs | Kagera Sugar FC | TBC | Azam Complex | Dar es Salaam |
| ROUND 30 | 233 | May 29, 2024 | Simba SC | vs | JKT Tanzania FC | TBC | TBC | |
| | 234 | May 29, 2024 | Coastal Union FC | vs | KMC FC | TBC | Mkwakwani Stadium | Tanga |
| | 235 | May 29, 2024 | Mashujaa FC | vs | Dodoma Jiji FC | TBC | Lake Tanganyika | Kigoma |
| | 236 | May 29, 2024 | Ihefu FC | vs | Mtibwa Sugar FC | TBC | Highland Estates | Mbeya |
| | 237 | May 29, 2024 | Young Africans SC | vs | Tanzania Prisons FC | TBC | TBC | |
| | 238 | May 29, 2024 | Namungo FC | vs | Kitayosce FC | TBC | Majaliwa Stadium | Lindi |
| | 239 | May 29, 2024 | Geita Gold FC | vs | Azam FC | TBC | Nyankumbu Stadium | Geita |
| | 240 | May 29, 2024 | Singida BS FC | vs | Kagera Sugar FC | TBC | Liti Stadium | Singida |
| FEDERATION CUP FINAL (02 JUNE 2024) | | | | | | | | |
| TFF AWARDS 2024 | | | | | | | | |
| FIFA INTERNATIONAL WINDOW (03 - 11 June) | | | | | | | | |
| PLAYOFF 2022/2023 ( PL vs PL) - LEG 1 &2 ( 04 - 08 JUNE 2024) | | | | | | | | |
| PLAYOFF 2022/2023 ( PL vs CL) - LEG 1 &2 ( 12 - 16 JUNE 2024) | | | | | | | | |

# Timu za Taifa za wavu zaingia kambi

**Na Wemael Mmaraba**

WACHEZAJI wa Timu za taifa za mpira wa wavu wameanza kambi kwa ajili ya michuano ya Mataifa ya Afrika ambayo yatafanyika nchini Cameroon.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Mpira wa Wavu Tanzania, amesema kambi hiyo imeanza mjini Dar es Salaam Agosti 6 mwaka huu ambapo timu zote mbili za ya wanawake na wanaume zimeanza mazoezi.

Mashindano hayo yatafanyika katika nchi mbili ambapo mbali na Cameroon, Misri pia imepewa uenyeji wa michuano hiyo mikubwa barani Afrika.

Mashindano ya Afrika yataanza Agosti 14. Kikosi cha wanawake ni Sara Hengama (KIUT), Gilda Loy Msechu (Pentagon), Jonia Jovin (JKT), Thabitha Laizer (JKT), Foibe Alex (jeshi Stars) na Christina Hosea (Star Girls).

Wengine ni Yasinta Remmy (Jeshi Star), Janeth Ajili (JKT), Mariam Omary(Star Girls), Lazia Mtandika (JKT), Naima Mrope(jkt), Jesca Peter (Jeshi Star), Dorolosa Revocatus (JKU), Neema Athumani(JKT) na Ester Noel (Magereza)

Kwa upande wa Wanaume ni Jovin Ngiriwa (KIUT), Nassoro Mohamed (JKT), Ezeckiel Rabson (JKT), Ramadhani Ramadhani (Jeshi Stars), Justus Makaya (High Voltage),Deodatus Muhandiki(Jeshi stars), Antony Oscar (Nyuki) na Stallone Wilbard (KIUT).

Wengine David Neeke (Kenya), Omar Bure (Rukinzo, Burundi), Michael Jovin (High Voltage), Lameck David (Jeshi stars), Ford Edward(High Voltage), Jackson Mmari (Ujerumani), Martin Anthony (KIUT), Khamis Sadalla (Mafunzo), Rashid Mustafa (JKTna Endrew Chogero (Mafunzo)

Leo yetu ndiyo kesho yetu
Uelekeo Spoti
| Jumatano Agosti 9 - 15, 2023 |



## Tottenham yakataa tena Ofa ya Bayern Munich

Uk. 22



# Yanga kuipasua tena Azam?

**Na Mwandishi Wetu**

MWISHO wa ubishi wa nani amesajili vizuri nani anakikosi kipana unaanza leo katika Uwanja wa Mkwakwani mjini Tanga, wakati mabingwa wa nagi wa Hisani, Yanga wakiwakaribisha Azam FC.

Mechi ya mwisho ya Kombe la Shirikisho baina ya timu hizo, ilishuhudia Azam wakifukuza benchi zima la ufundi lililokuwa likiongozwa na mshambuliaji wa zamani wa Yanga, Kalimangonga Ongalla 'Kally' na msaidizi wake Aggrey Morris.

Inaendelea Uk.23



## Ramos sasa ajiunga PSG

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI hatari, Gonçalo Ramos amesaini Mkataba wa mkopo wa Mwaka mmoja na Klabu ya Paris Saint-Germain akitokea Benfica ya Ureno.



## Nabi, Kaze 'walifukuzwa kazi'

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Nasredine Nabbi alifungasha mizigo yake yote akijiandaa kutimuliwa na klabu ya Yanga wakati wakienda kucheza mechi ya marudiano na Club Africain ya Tunisia katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Inaendelea Uk.23



Uk.23

## Singida FG, Ruffo wamgeukia msichana



**Na Valensi Mbaga,TUDARCo**

TIMU za Singida Fountaln Gate na Fountain Gate Princess, kwa kushirikiana na Taasisi ya Raising Up Friendship Foundation (RUFFO), zimezindua mradi la 'Usawa Mpirani'.

Inaendelea Uk.23



## Bondia Grace Mwakamele atwaa Medali ya Fedha